epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Ijumaa Novemba 15, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581861
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

UCHAGUZI WA MITAA...

# CCT yaibuka na hoja nne

• **Yaacha** angalizo "yasijirudie ya mwaka 2019"...*Uk.2*



Mwenyekiti wa CCT, Askofu Dk. Fredrick Shoo



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akitoa heshima za mwisho kwenye jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Marehemu Lawrence Mafuru katika viwanja vya Karimjee Jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**



# Rais ataja mawili ya Mafuru yatabaki kumbukumbu kwake

UKURASA 2

## CHADEMA yatolea ufafanuzi hoja mbili zilizozua mjadala

UKURASA 3

UKURASA WA 4

**Waziri:** Makundi haya yana hali mbaya ushamiri wa VVU nchini



UKURASA WA 4

**Raia** wa kigeni kizimbani kwa shtaka kuingilia mifumo ya benki

UKURASA WA 19

**Viongozi** wa dini Afrika wakutana, wataka udhibiti maombezi feki



Skani hapa kutembelea chaneli yetu

# Samia ataja mawili ya Mafuru yatabaki kumbukumbu kwake

**Na Restuta James**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemlilia aliyekuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, marehemu Lawrance Mafuru, na kueleza namna alivyoisaidia nchi katika nyakati mbili ngumu.

Amezitaja kuwa ni wakati wa tatizo la uhaba wa dola uliomlazimu kuunda kamati akiwamo Mafuru na nyingine iliyohusu ujenzi wa miradi na kutoa ushauri chanya uliosaidia kukwamua masuala hayo.

Rais Samia aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, katika shughuli ya kuaga mwili wa Mafuru, aliyefariki dunia kwa ugonjwa wa saratani ya damu.

Alisema aliposikia Mafuru amefariki, alikumbuka alivyofanikisha kutatua tatizo la uhaba wa fedha za kigeni nchini, takribani mwaka mmoja uliopita.

Mwaka jana, Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ililazimika kuuza Dola za Marekani milioni mbili kwa benki kila siku, ili kukabiliana na uhaba wa sarafu hiyo nchini. Uhaba huo ulisababisha baadhi ya wafanyabiashara, kuiuza kinyemela kwa bei ya ulanguzi.

"Tulipopata changamoto ya dola ndani ya nchin, niliunda kamati ambayo iliongozwa na (Nehemia) Mchechu akisaidiwa na Mafuru. Kamati ilifanya kazi kubwa na siku ya kufanya wasilisho mbele yangu, kuweka mpango mezani wa kuleta dola ndani ya nchi, Mafuru aliniambia, Mheshimiwa tukiufuata mpango huu, kama tulivyouleta nchi itaondokana na tatizo hili si muda mrefu.

Na leo wote ni mashahidi, badala ya kuzibembeleza benki kutupa dola, sasa zinatuita tukachukue dola kwao. Badala ya kulalamika nchi haina dola, nimesikia juzi wazalishaji wanalalamika, nchi haina shilingi," alisema Rais Samia.

Alisema kwa kuwa Mafuru ameondoka, atawatumia wataalamu wengine kurejesha shilingi kwenye mzunguko wa uchumi.

"La pili, tulikumbwa na changamoto ya miradi katika sekta ya ujenzi na nikaita mkutano pale Zanzibar, katika kikao kile tulijadili mengi.

"Mwisho nikawaambia, katika hali kama hii tuliyofika, kati yenu mmoja angekuwa Rais, mngeamuaje? Nikasema leo najivua urais, ninampa Lawrance Mafuru na nikamwambia, Lawrance nyanyuka, wewe sasa ndiye Rais, ungefanyaje?

"Alisimama kwa unyenyekevu mkubwa, akaniambia mimi siyo Rais na urais uko mbali na mimi, lakini katika hali kama hii, akatoa mchango wake ambao hakika ulitutoa pale tulipokuwa na tukaweza kusonga mbele. Ndugu zangu, nimepoteza, tumepoteza kwenye taifa hili," alisema Rais Samia.

Mbali ya kumsadia katika nyakati hizo mbili, Rais Samia alisema Mafuru alikuwa mshauri wake binafsi hata kabla hajamteua kusimamia taasisi za umma.

Alisema mwaka jana alimteua kuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, nafasi aliyoishika hadi alipopatwa na umauti, kazi aliyoifanya kwa uaminifu ndani ya mwaka mmoja.

Alisema hadi umauti unamkuta, Mafuru alikuwa anasimamia dhamana ya kuandika Dira ya Taifa ya Maendeleo (Vision 2050), ambayo wiki hii amekabidhiwa rasimu ya kwanza.

Alisema katika utumishi wa umma akianzia Hazina, Mafuru alifanya mageuzi na kuweka mifumo ya kitaasisi, ambayo yameendelea kufanyika kwa manufaa ya nchi.

Aliwashauri watumishi wa umma na sekta binafsi, kujifunza uchapakazi, ubunifu na uaminifu wake, kwa kutoa mchango wao wote katika nafasi wanazopewa ili kuacha alama chanya.

Awali, Msajili wa Hazina, Nehemia Mchechu, alisema Mafuru ndiye aliyefanya maboresho makubwa ya muundo wa ofisi hiyo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema Mafuru alitoa mchango mkubwa kwa taifa na amefariki dunia bila deni, kwa kuwa alitumia karama alizopewa na Mungu kujenga familia na nchi.

Dk. Mkumbo alisema katika kuandika Dira ya 2050, walizungumza na Mafuru akiwa hospitalini India na kuweka maoni yake ukurasa kwa ukurasa wa rasimu hiyo.

Akisoma wasifu wa Mafuru, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Dk. Tausi Kida, alisema alizaliwa Juni 20, 1972 mkoani Mara na kusoma shule za msingi na sekondari hapa nchini, kisha kujiunga Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hadi ngazi ya shahada ya uzamili katika usimamizi wa biashara.

Alisema amefanyakazi sekta binafsi kwenye benki kadhaa hadi mwaka 2016, alipoteuliwa kwenye utumishi wa umma, akiwa Msajili wa Hazina.

Alisema Mafuru alianza kuugua saratani ya damu Agosti mwaka huu na kutibiwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), kisha akahamishiwa Apollo nchini India, ambako alipoteza maisha akiwa na umri wa miaka 52.

Katika ibada hiyo ya kitaifa, iliongozwa na Askofu Mkuu wa Kanisa la Waadventista Wasabato (SDA), Jimbo la Kaskazini mwa Tanzania, Mchungaji Mark Malekana, aliwakumbusha waumini kwa Zaburi ya 90:1-3.

Viongozi wengine waliohudhuria ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, mawaziri, makatibu wakuu, manaibu Spikawa Bunge, wafanyabiashara, Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete na Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda.

Akitoa salamu za familia, mdogo wake, Maendeka Mafuru, aliishukuru serikali, Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Prof. Mohamed Janabi na watumishi wa Idara ya Dharura hospitalini hapo, kwa namna walivyopambana kuokoa maisha yake na kuushukuru ubalozi wa Tanzania nchini India, kwa namna walivyokuwa sehemu ya familia.



Spika wa Bunge na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Dk Tulia Ackson akizungumza katika mkutano wa Maspika wa Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Nairobi nchini Kenya juzi. Katika Mkutano huo, Dk Tulia alikabidhi nafasi ya Mwenyekiti kwa Spika wa Bunge la Kenya Moses Wetang'ula. **PICHA: BUNGE**

# CCT yaibuka na hoja nne uchaguzi mitaa

**Na Maulid Mmbaga**

JUMUIYA ya Kikristo Tanzania (CCT) imeibua hoja nne, ikiwamo kuvisisitiza vyombo vya dola kuwa haitarajii kuona yaliyotokea katika uchaguzi wa mwaka 2019/20 yakijirudia tena.

Kwa mujibu wa jumuiya hiyo, Watanzania wana haki ya kugombea nafasi za uongozi na kuwachagua viongozi wanaowataka bila shinikizo lolote.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa CCT, Askofu Dk. Fredrick Shoo, alisema wameendelea kushuhudia siku za karibuni watu kupotea na wengine kuuawa kuelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, hivyo wanakemea vitendo hivyo na kuzitaka mamlaka husika kufanya ufuatiliaji wa kina utakaosaidia kupatikana majibu ili kuondoa taharuki na hofu iliyoko kwenye jamii.

Pia alisisitiza umuhimu wa uchaguzi wa serikali za mitaa kusimamiwa na na kufanyika kwa haki na usawa, pamoja na kufanyika marekebisho ya katiba ili kuondoa changamoto zinazoathiri mchakato wa uchaguzi kila wakati.

"Kumekuwapo na malalamiko kuwa baadhi ya wagombea hususani wa vyama vya upinzani wamewekewa vikwazo. Baadhi ya ofisi zimekutwa zimefungwa wakati wa kurudisha fomu na fomu nyingi hazikubandikwa au zimebandikwa vibaya na kusababisha kuharibika au kutodumu kwa muda mrefu kwenye mbao za matangazo.

"Pia tumeshuhudia changamoto katika mchakato wa kukata rufani ambako siku ya kupokea rufani baadhi ya wasimamizi walifunga ofisi na kuzuia mapingamizi mengi, jambo linalosababisha malalamiko miongoni mwa wagombea.

Tunasisitiza kwamba kuelekea uchaguzi mkuu wa 2025, kama hakutachukuliwa hatua stahiki kutakuwa na changamoto zile zile katika chaguzi zijazo," alisema Askofu Dk. Shoo.

Alisisitiza wananchi kwamba ni muhimu kufuatilia kampeni kwa makini na kuchagua viongozi wanaoonekana kuleta maendeleo ya kijamii pamoja na kudumisha amani na utulivu kabla, wakati na baada ya uchaguzi.

Pia alihimiza wananchi kuepuka vishawishi vyovyote vya kiitikadi au namna yoyote inayoweza kusababisha uvunjifu wa amani pamoja na kumtanguliza Mungu katika kipindi hiki muhimu cha uchaguzi kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa taifa.

Wakati huo huo, alishauri mamlaka husika kwamba endapo mgombea hana mpinzani sheria inaelekeza apigiwe kura ya NDIYO au HAPANA ili kutoa haki kwa wananchi kuchagua viongozi wanaowataka.

Hata hivyo, alisisitiza vyama vya siasa kufuatilia na kusimamia kampeni za wagombea kutoka katika vyama vyao na kuhimiza ustaarabu na kuheshimiana katika kunadi sera za chama husika bila kutumia lugha mbaya za matusi au maudhi zinazoweza kuhatarisha amani ya nchi.

"Tunahamasisha vyama vyote vinavyowania nafasi za uchaguzi kuweka mawakala waadilifu katika kusimamia upigaji kura, kuhesabu, kujumlisha na kutangaza matokeo ili kuepuka sintofahamu baada ya uchaguzi na kutupeana lawama.

"Tunatoa wito kwa wasimamizi wa uchaguzi kutekeleza majukumu yao kwa uwazi, usawa kwa kuzingatia sheria zilizowekwa bila upendeleo wa aina yeyote. Tunatumia fursa hii kuishauri wizara husika kuwachukulia hatua pale inapothibitika wasimamizi wamefanya kwa makusudi au kwa uzembe. Hii itasaidia kurejesha imani kwa wananchi," alisema.

Kuhusu kampeni za wagombea, Askofu Shoo alihimiza mamlaka na vyombo vyote vinavyohusika kutoa nafasi sawa kwa vyama vyote vya siasa vinavyogombea kufanya mikutano yao kwa uhuru na usawa bila kubughudhiwa.

Pia alihimiza viongozi na wahusika wote kudumisha uwazi katika hatua ya kuhesabu na kujumlisha kura kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizowekwa bila upendeleo ili kudumisha amani baada ya uchaguzi.

Alisisitiza kuwa mamlaka husika kuzingatia usawa na uwazi katika kutangaza matokeo halisi ya uchaguzi kwa mujibu wa muda uliowekwa na bila ucheleweshaji wowote ambao mara nyingi husababisha kukosekana kwa imani na matokeo husika.

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

## HABARI KITAIFA

## Adaiwa kumuua baba mkwe madai kutotatua mgogoro wa ndoa yake

**Na Mary Mosha,** MOSHI

JESHI la Polisi mkoani Kilimanjaro linamshikilia Deogratias Mbuya (40), mkazi wa kijiji cha Legho Kilema, wilayani Moshi kwa tuhuma za kumuua baba mkwe, Tibrus Mneney (72) kwa madai ya kushindwa kutatua mgogoro wa ndoa.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Simon Maigwa alisema tukio hilo lilitokea juzi mchana nyumbani kwa baba mkwe wa Mbuya katika kijiji hicho, kata ya Kilema Kusini.

Alisema ugomvi huo ulitokea wakiwa katika kikao cha usuluhishi cha familia ya mtuhumiwa na mke wake baada ya kukosa suluhisho, alimkatakata Tibrus na kitu chenye ncha kali katika maeneo ya shingoni, kichwani na mkononi na kusababisha kuvuja damu nyingi na kupoteza maisha.

"Mtuhumiwa alikuwa na mgogoro wa ndoa na mkewe, akimtuhumu kutoka nje ya ndoa mara baada ya kufanyiwa upasuaji kutokana na matatizo ya kiafya.

"Baada ya kushindwa kupata suluhisho, alianza kumpiga mama mkwe wake, Biritha Mneney (58) ndipo baba mkwe Tibrus Mneney alipoingilia kati na kukatwakatwa," alisema Kamanda.

Alisema kuwa mara baada ya mtuhumiwa kutekeleza tukio hilo, alitoroka hadi jana alipokutwa katika nyumba bovu ya Revocatus Mbuya, akiwa hawezi kuongea na sasa amelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda (KCMC) kwa matibabu.

Wakati huo, Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wa tukio la kudaiwa kujinyonga, fundi magari Hassan Mwanga (39), mkazi wa Pasua, ambaye mwili wake umekutwa pembeni ya uwanja wa mpira wa Mandela wilayani Moshi ukiwa chini na unakamba ya katani shingoni.

# CHADEMA yatolea ufafanuzi hoja mbili zilizozua mjadala

**Na Elizabeth Zaya**

UONGOZI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) umetoka hadharani kujibu hoja mbili zilizoibuliwa hivi karibuni, yakiwamo madai ya "kuwapo fedha chafu ndani ya chama hicho", ukiwataka wenye ushahidi kuwasilisha. Mbali na tuhuma za kuwapo fedha chafu, chama hicho kimepinga vikali madai kwamba viongozi wake wa juu wamefanya makubaliano ya siri ili kigawiwe madaraka kwenye muundo wa serikali au kipewe majimbo katika uchaguzi ujao.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, kuibuliwa madai hayo kumesababisha wanachama, wapenzi wa chama hicho na wananchi kwa ujumla kutaka ufafanuzi rasmi. "Hivi karibuni kumeibuka tena wimbi la hoja mbalimbali ambazo zilishawahi kuibuka siku za nyuma na ambazo zimesababisha wanachama, wapenzi wa CHADEMA na wananchi kwa ujumla kutaka ufafanuzi rasmi wa chama,"alisema Mrema.

Akijibu hoja hizo, Mrema alisema tuhuma za CHADEMA kuwa na fedha chafu au rushwa katika uchaguzi wa ndani wa chama, zimekosa ushahidi na maeneo mengine uchunguzi bado unaendelea.

"CHADEMA imekuwa mstari wa mbele kupambana na ufisadi, ubadhirifu na rushwa miaka yote. Kama chama kikiletewa ushahidi au vielelezo vya tuhuma hizo kutoka kwa mtu yeyote, tutafanyia kazi haraka iwezekanavyo kwa mujibu wa Katiba, kanuni na mwongozo wa chama dhidi ya rushwa wa mwaka 2012.

"Hivyo, tunamwalika mtu yeyote mwenye ushahidi au vielelezo vinavyotosheleza kuwezesha kuchukua hatua za kinidhamu kwa wahusika, awasiliane na Ofisi ya Katibu Mkuu au Ofisi ya Katibu yeyote wa kanda," alisema Mrema.

Akifafanua kuhusu hoja ya viongozi wa juu wa chama hicho kudaiwa kukaa vikao vya siri, Mrema alisema ni vema ikaeleweka kuwa kwa mujibu wa Katiba ya nchi, nafasi za juu za uongozi wa nchi, ikiwamo ya Makamu wa Rais, hugombewa na haitolewi mezani.

Alisema kuwa nafasi ya Waziri Mkuu hutokana na chama chenye wabunge wengi bungeni.

"CHADEMA katika vikao vyake vyote, haijawahi kujadili, kutoa au kupokea mapendekezo yoyote ya kitu kinachoitwa 'Serikali ya nusu mkate'. Jambo hili kama linavyopotoshwa, halijawahi kuwa sera ya chama chetu. Hakijawahi kupokea, kujadili, kubeba au kuwa na ajenda na serikali katika vikao vyote vya chama au vile vya maridhiano kuhusu hoja tajwa.

"Ikumbukwe kuwa vikao vyote vya maridhiano vilifanyika mwaka 2022 na vikahitimishwa Januari mwaka 2023, ambapo Rais Samia Suluhu Hassan aliondoa katazo la shughuli za kisiasa, ikiwamo mikutano ya hadhara na maandamano. Na ni 30 na 31 palifanyika vikao vya mwisho ambapo tulishindwana, baada ya hapo hakuna kikao cha siri au hadharani kimefanyika baina ya CCM na CHADEMA," alifafanua.

Mrema alisema kuwa kwa kipindi chote cha mwaka 2023 na 2024, chama hicho kimekuwa katika programu mbalimbali zenye lengo kukihuisha kufuatia miaka saba ya kuzuiwa mikutano ya hadhara.

Kuhusu ajenda ya Katiba mpya, na madai ya mfumo huru wa uchaguzi, Mrema alisema hazijawahi kuachwa na chama hicho wakati wote wa kutekeleza programu zake kwa sababu yoyote ile kama inavyotaka kuaminishwa. "Tunawasihi wanachama na wapenzi wetu waendelee kukilinda na kukijenga chama kirejeshe heshima yake iliyoporwa, tunawataka wanachama na viongozi wetu, kuwekeza nguvu katika uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji, vitongoji na kupuuza propaganda za kukigawa chama," alisema.

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu Na. 126 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392 na Kanuni Na. 5(1) ya Kanuni za Mafuta (Compressed Natural Gas) (Supply and Marketing Services Rules, GN No. 220 of 2019).**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji **(EWURA)** imepokea ombi kutoka kwa **PUMA ENERGY TANZANIA LIMITED** ya kibali cha ujenzi wa kituo kidogo cha kupokea gesi asilia iliyoshindiliwa kitakacho jengwa kiwanja namba mbili (02) eneo la kiwanda cha **ALLIANCE ONE TOBACCO (T) LIMITED** kilichopo kata ya Kingolwira, Wilaya ya Morogoro Vijijini, mkoani Morogoro. Gesi asilia hii itatumika kama nishati kwenye kiwanda cha **ALLIANCE ONE TOBACCO (T) LIMITED** kuendeshea boiler, forklift na kuzalisha umeme.

Hivyo, mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya ombi tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya tangazo hili.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli**
**S. L. P 2857, Dodoma.**
Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;
Namba ya Bure 0800110030;
Barua pepe: **info@ewura.go.tz** Tovuti: **http://www.ewura.go.tz**

**Imetolea na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go tz



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu Na. 126 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392 na Kanuni Na. 5(1) ya Kanuni za Mafuta (Compressed Natural Gas) (Supply and Marketing Services Rules, GN No. 220 of 2019).**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea ombi la kibali cha ujenzi wa kituo cha kujaza gesi asilia iliyoshindiliwa kwenye magari kutoka **RAFIKI CNG STATION AND CONVERSION CENTRES LIMITED** kitakachojengwa kandokando ya barabara ya Nelson Mandela, kiwanja namba **P47814** eneo la Mabibo Farasi, Kata ya Mabibo, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam.

Hivyo, mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya ombi tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha **EWURA** kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya tangazo hili.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli**
**S. L. P 2857, Dodoma.**
Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;
Namba ya Bure 0800110030;
Barua pepe: **info@ewura.go.tz** Tovuti: **http://www.ewura.go.tz**

**Imetolea na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go tz

# Makundi sugu maambukizi VVU yatajwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MADEREVA wa masafa marefu, wachimbaji wadogo wa madini, wavuvi na vijana wa umri wa miaka 15 hadi 24, wametajwa kuwa ni miongoni mwa makundi ambayo bado yana maambukizi mapya makubwa ya Virusi vya Ukimwi (VVU).

Kutokana na hali hiyo, serikali imewasihi wananchi wote kujikinga na kutumia dawa kwa usahihi kwa wale waliojitambua wanaishi na maambukizi.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga, aliyasema hayo jana jijini hapa kuhusu kuelekea maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani mwaka 2024.

Alisema kwa mujibu wa matokeo ya utafiti wa viashiria vya Ukimwi wa mwaka 2022/23, makundi hayo bado yanaongezeko la kushamiri kwa maambukizi mapya.

Pia alisema utafiti huo umeonesha mafanikio mbalimbali ikiwamo idadi ya watu wanaoishi na VVU kuwa ni 1,540,000 kulinganisha na takriban watu 1,700,000 mwaka 2016/17.

"Ushamiri wa Virusi Vya Ukimwi (VVU) kitaifa ni asilimia 4.4 ikilinganishwa na asilimia 4.7 kwa mwaka 2016/17," alisema.

Alitoa wito kwa wanajamii na wadau kushirikiana katika kupanga na kutekeleza shughuli za kudhibiti VVU na Ukimwi kwa kuzingatia vipaumbele na mahitaji ya mahali walipo.

"Katika utekelezaji wa hilo, usawa hasa wa kijinsia na katika utoaji huduma kwa misingi ya haki ni nguzo kubwa katika kutimiza ndoto yetu ya kumaliza VVU na Ukimwi ifikapo mwaka 2030," alisema.

Alitaja maeneo ya kipaumbele ni pamoja na kuimarisha afua za VVU na Ukimwi kwa vijana kwa kuwa takwimu zinaonesha kuwa kundi la vijana wenye umri huo linachangia kwa kiwango kikubwa maambukizi hayo. Kuhusu Siku ya Ukimwi Duniani, alisema kitaifa itafanyikia Ruvuma na kuanzia Novemba 24, 2024 kutakuwa na huduma ya upimaji wa hiari wa VVU kwa wiki nzima hadi Desemba Mosi. Huduma hizo na zitatolewa kwenye mabanda ya maonesho yatakayokuwa kwenye uwanja wa michezo wa Majimaji. Alisema pia kutakuwa na mdahalo wa vijana na viongozi wa kidini na wa kimila na siku ya kilele na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), Dk. Jerome Kamwela, alisema mikakati imeandaliwa kukabiliana na hali maambukizi mapya ikiwamo utoaji huduma na elimu kupitia programu mbalimbali.

Alisema kuna miradi ambayo inahakikisha huduma zinafika katika maeneo ya wavuvi hasa kwenye mialo na visiwani kwa kuweka huduma za mkoba ili kutoa huduma.

"Madereva wa masafa marefu magari yanayopita yanatoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda mpaka Rawanda, Burundi kwenda Kongo kwa korido ya katikati inayopita Dodoma kutoka Dar es Salaam.

"Kuna vituo vya huduma vipo pembeni ya barabara ambavyo vimewekwa mahsusi maeneo ambayo wenzetu wa masafa marefu wanapumzika, ili anayetumia dawa aweze kupata huduma na anayehitaji kujua afya yake, aweze kupata huduma hiyo na tumefanya hivyo hata kwa barabara ya kutoka Dar es Salaam hadi Tunduma."

"Tuna vituo 21 vinavyotoa huduma kama hiyo kwa hiyo kila kundi kuna mkakati ambao unaangalia mahitaji ya kundi maalum tofauti na huduma tunayotoa kwenye jumuiya na katika jamii yetu," alisema.

Alisema kwa sasa wanajitahidi kufanya kwa kuwapelekea huduma waliko hasa wanaume na vijana, ndio maana shuleni kuna klabu za vijana za afya na masuala ya UKIMWI.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Watu Wanaoishi na VVU (NACOPHA), Emanuel Msinga, aliwaasa watanzania kujenga utamaduni wa kupima VVU ili watakapobainika kuwa na maambukizi waanze dawa mapema.

Awali, Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Ukimwi la Umoja wa Mataifa (UNAIDS), Dk. Martin Odiit, alipongeza jitihada za Tanzania katika kukabiliana na ugonjwa huo ili kufikia lengo la 0-0-0 ifikapo Mwaka 2030.



Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri (aliyesimama) akizungumza kwenye Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP29) unaofanyika jijini Baku nchini Azerbaijan ambao Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango (hayupo pichani) aliongoza ujumbe wa Tanzania uliowakilishwa na mashirika ya WaterAid, UNICEF, NDC Partnership na Climate Action Network Tanzania ambayo ni miongoni mwa mashirika na taasisi nyingine za kimataifa katika kushirikiana na Serikali kwenye kutekeleza malengo ya maji kupitia Mpango wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (NDC). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kizimbani madai kuingilia mfumo wa benki

**Na Grace Gurisha**

RAIA wa Malawi, Hapi Shora, maarufu kwa jina la Showshow (54), amependishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, na wenzake wawili kwa tuhuma za kuingilia mfumo wa kompyuta wa benki ya CRDB kwa nia ya kuiba fedha.

Mbali na Shora, washtakiwa wengine ni Joseph Wasonga (53) mfanyabiashara Mkazi wa Mikocheni B na Franco Luhinda (41) mfanyabiashara na Mkazi wa Tabata, Dar es Salaam.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali, Eric Davis, alidai juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Godfrey Mhini kuwa washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka mawili. Wakati wa kusoma mashtaka, Wakili aliomba asome kwa lugha ya Kiswahili na kutafsiri kwa lugha Kingereza kwa ajili ya Shora.

Wakili Davis alidai kuwa shtaka la kwanza linalowakabili ni kuongoza genge la uhalifu ambalo linawakabili washtakiwa wote kwa madai kuwa tarehe zisizohamishika wakiwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa makusudi, waliongoza genge la uhalifu.

Ilidaiwa kuwa washtakiwa waliongoza genge hilo kwa kuingilia mfumo wa kompyuta wa CRDB kwa nia ya kuiba fedha kinyume cha sheria.

Katika shtaka la pili, alidai kuwa washtakiwa kwa pamoja wanatuhumiwa kwa jaribio la kutenda kosa Oktoba 30, 2024 wakiwa jijini Mwanza ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwamba walifanya jaribio la kutenda kosa la kuingilia mfumo wa kompyuta wa CRDB.

Alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa ili kuangalia hatua ya upelelezi ilipofikia. Hakimu Mhini alisema mashtaka hayo si miongoni mwa makosa ambayo hayana dhamana, hivyo kutoa masharti kwa washtakiwa wote.

Alisema ili wawe nje kwa dhamana, washtakiwa wanatakiwa kuwa na wadhamini wawili wenye barua za utambulisho kutoka serikali za mitaa na pia wawe wakazi wa Dar es Salaam wenye shughuli zinazofahamika.

Pia alisema wadhamini hao wanatakiwa wawe na vitambulisho vya taifa (NIDA) na washtakiwa wanatakiwa wawasilishe mahakamani hati zao za kusafiria na wakitaka kutoka nje ya mkoa wa Dar es Salaam, lazima wapate kibali cha mahakama. "Kila mdhamini atatia saini bondi ya Sh. milioni tano," alisema Hakimu Mhini.

Hata hivyo, Wakili Davis alipinga washtakiwa hao kupewa dhamana kwa sababu hawana uhakika kama ni kweli hati zao waliziwasilisha kituo cha polisi, hivyo lazima wajiridhishe.

Pia alidai baadhi wadhamini hawajakidhi vigezo kwa sababu wengine wametoka nje ya mkoa wa Dar es Salaam na wengine hawana vitambilisho vya NIDA.

"Nimekubaliana na ombi la upande wa mashtaka la kutokutoa dhamana kwamba ni lazima wajiridhe kwanza kama hati hizo kweli ziko kituo cha polisi, washtakiwa watarudi rumande hadi Novemba 26,2024," alisema Hakimu Mhini

## Bidhaa bandia bado mfupa mgumu

**Na Romana Mallya**

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Balozi Dk. John Simbachawene, amesema bidhaa bandia na hafifu bado zimo katika masoko nchini na kwamba hilo bado ni tatizo.

Amesema pamoja na kushamiri huko, jitihada zimefanyika kupunguza na kumekuwa na mafanikio kwa kuhamasisha wazalishaji wa bidhaa kutumia mifumo ya SCANCODE na kutengeneza mifumo yenye uwezo wa kusimamia mikutano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa.

Balozi Simbachawene aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya wabunifu wa mifumo ya kudhibiti bidhaa bandia sokoni na maadhimisho ya miaka 10 ya mfumo huo.

Alitoa rai kwa taasisi za serikali zinazohusika na ukuaji na uendelezaji wa wajasiriamali kushirikiana na taasisi binafsi ili kufikia malengo yaliyowekwa.

Kadhalika, alitaka serikali za mitaa, maofisa biashara na maofisa maendeleo ya jamii kuendelea kuhimiza ukuaji wa wajasiriamali hasa kwa kutumia huduma hizo za kisasa katika kupunguza bidhaa bandia, kupunguza upotevu wa mapato na kuwasiliana ili kusaidia kutanua zaidi wigo wa masoko ya ndani na nje.

Alisema serikali ina malengo mahususi ya kusaidia makundi mbalimbali ya jamii yakiwamo ya wajasiriamali wanawake, vijana na makundi maalumu kwa kutenga fedha kusaidia kupata mitaji ya kuendeleza na kuwezesha shughuli za ujasiriamali nchini.

"Wananchi kwenye maeneo yetu ni lazima kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan kwa kufanya kazi kwa bidii zaidi na kwa ubunifu zaidi kulingana na mazingira ya sasa ya matumizi ya teknolojia.

"SCANCODE kwa kushirikiana na SIDO (Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo) wameonesha njia ya namna ya kumuunga mkono Rais Samia katika kujikwamua kiuchumi," alisema.

Alisema ili kuonesha kujali, kuheshimu na hata kuthamini juhudi zake, watumie kila fursa iandaliwayo na serikali na kuileta kwao ili wanufaike na kujenga zaidi uchumi wa mtu mmoja mmoja na kwa taifa zima.

Mkurugenzi Mkuu wa SCANCODE (T) Ltd, Faustine Mgimba, aliiomba serikali katika kupunguza matumizi ya mifumo ya nje inayoweza kuwa hatarishi kwa taifa, wahamasishe utumiaji ya mifumo ya ndani.

Alisema ili kufikia lengo la Rais Samia la kuwainua wajasiriamali, wanaomba viongozi wa serikali kutangaza matumizi ya mfumo wa SCANCODE na umuhimu wake kwa sekta ya viwanda na biashara ili huduma zijulikane kikamilifu.

Mgimba aliomba huduma za mfumo huo kwa kuwa ni mpya, zijumuishwe katika sera na miongozo, kanuni na sheria kadri inavyofaa hadi katika mamlaka za serikali za mitaa na kutoa elimu kwa maofisa biashara wote ili kusisitiza umuhimu wake katika kudhibiti bidhaa bandia katika mashirika, taasisi na huduma.

# MATANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA KUONESHA NIA: UTOAJI MSAADA WA HUDUMA YA MANUNUZI, UGAVI NA USAFIRISHAJI WA VIPURI VYA MATENGENEZO, NA VIFAA VINGINE VYA MATUMIZI YA AWALI KWA AJILI YA EACOP: KUMBUKUMBU NA. REQ-00000659

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD ("EACOP LTD") linakaribisha kampuni yenye uzoefu na weledi wakutosha kuonesha nia ya kutoa Msaada wa Huduma ya Manunuzi, Ugavi na Usafirishaji wa Vipuri vya matengenezo, na vifaa vingine vya matumizi ya awali kwa ajili ya EACOP kwa ajili mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP)

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini ya ardhi linalovuka mpaka ili kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda hadi pwani ya mashariki mwa Tanzania kwa ajili ya kusafirisha katika masoko ya kimataifa. Bomba hilo litaanzia Kabaale wilayani Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania. Urefu wa bomba hilo ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania. Bomba hilo litapita katika mikoa minane (8) inayojumuisha Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga, Halmashauri za Wilaya 27 za Tawala na Vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) utahitaji suluhisho Madhubuti ili kusaidia utayari wake wa utendaji wa shughuli katika Kituo cha Kuhifadhia Mafuta Baharini (MST), Tanga, Tanzania. Huduma hii inapaswa kujumuishavipengele vifuatavyo.

Kamasehemu ya dhamira ya kampuni ya kukuza watoa huduma wa ndani na ushiriki wa Raia wa Tanzania katika mnyororo wa thamani wa Mafuta na Gesi, EACOP inatafuta huduma za makampuni yanayotambulika na yenye sifa na uzoefu wa kutoa huduma za manunuzi kwa ajili ya ununuzi na usafirishaji wa vipuri kwa ajili ya matengenezo na manunuzi vifaa vya awali vya matumizi ili kusaidia Uendeshaji wa shughuli katika eneo la kazi. Kulingana na orodha ya vipuri iliyotolewa na mkandarasimkaguzi wa uhandisi, mtoa huduma atasimamia:

- Mchakato wa manunuzi,
- Vifaa na huduma zinazohusiana na maombi au oda iliyotolewa,
- Utoaji wa eneo la kuhifadhia na
- Kuwasilisha kwenye ghala la EACOP la kituo cha Tanga na kuingiza data/taarifa husika kwenye mfumo wa KAMPUNI.

Malengo ya EOI hii ni kutafuta mkandarasi anayeweza kutoa huduma Madhubuti ya ununuzi na usafirishaji ili kusaidia utoaji wa huduma ya matengenezo, unaojumuisha aina mbalimbali za kazi muhimu, ikiwa ni pamoja na:

**USIMAMIZI WA NYARAKA**
- Usimamizi wanyaraka za mzabuni, vyeti , na rekodi au taarifa zinazohusiana.

**HUDUMA ZA MANUNUZI**
- Utayarishaji wa Mkataba na /au agizo la Ununuzi, mapitio ya zabuni, ufafanuzi, tathmini na masuala ya mapendekezo.
- Usimamizi kamili wa manunuzi, ikijumuisha usambazaji wa vifaa, zana na vipuri muhimu.
- Utoaji wa vipuri na vifaa vya matumizi kwa ajili ya uendeshaji wa awali na matengenezo yanayoendelea ya mtambo.
- Usimamizi Madhubuti wa mikataba na viambatishi vyake

**HUDUMA ZA USAFIRISHAJI**
- Usafirishaji na utunzaji wa mizigo hadi mwisho.
- Upakiaji, ufungaji, upakuaji na upangaji wa mzigo.
- Ushughulikiaji wa mizigo na Usaidizi wa kutoa mizigo ya wateja bandarini
- Uhifadhi wa mizigo inayoingia.
- Usimamizi wa Leseni zinazohitajika za uagizaji mizigo (ikijumuisha nyaraka za uagizaji bidhaa, PVoC, GCLA n.k.).
- Mfumo wa usimamizi wa ghala ili kuhakikisha uhifadhi ulioboreshwa.

**HUDUMA ZINAZOHITAJIKA**
- Ukusanyiko wa vifaa kutoka eneo kwa mzabuni
- Usafirishajiwa baharini na nchi kavu (ikiwa ni pamoja na usafirishaji wa ndani ya nchi).
- Masharti ya dhamana ya Usafirishaji: kutoka kwa DAP mpaka kwenye maghala ya kampuni katikaVituo vya Baharini, Tanga.
- Ukaguzi, upimaji, na usimamizi wa bima.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**KUHIFADHI, KUTUNZA, KULINDA**
- Utoaji wa miundombinu ya kuhifadhia ya muda kama inavyohitajika.

**UCHAKATAJI WA DATA MAPOKEZI**
- Usajili wa bidhaa zilizopokewa ndani ya mfumo wa ERP wa KAMPUNI.

**VIGEZO MUHIMU:**
Makampuni au taasisi zinazoonesha nia zinakaribishwa kutuma maombi kwa kuambatanisha nyaraka zifuatazo:
- Maelezo mafupi yanayoonesha uzoefu wa kufanya shughuli kama hizo.
- Uzoefu bayana wa kufanya shughuli kama hizo kwa ufanisi katika usaidia wa miradi mikubwa.
- Uthibitisho wa uzoefu wa angalau miaka 6 katika kutoa huduma sawa hii kwa miradi au makampuni yanayohusiana ikijumuisha barua za uthibitisho kutoka kwa wateja watatu wa hivi karibuni .
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi cha mwaka huu. (Ambatanisha nakala).
- Nakala ya ripoti rasmi ya Kampuni kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni toka BRELA. (Ambatanisha nakala).
- Cheti cha usajili na leseni ya Biashara. (Ambatanisha nakala).
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za miaka mitatu iliyopita.
- Wasifu wa watendaji wakuuwatakaohusika katika utoaji wa Huduma ikiwa ni pamoja na vyeti vyao, kiwango cha uhitimu, uzoefu na uwezo wa kutoa huduma zinazohitajika katika miradi mikubwa.
- Uthibitisho kutoka kwenye mfumo wa Usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na Viwango vya Ndani na vya Ki-Sekta vinavyotumika kwa kazi zinazofanana na hii.
- Uthibitisho wa kukubaliana nasera za kupinga rushwa, ufisadi, naSera YA Haki za Binandamu.
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha wamesajiliwa au kuonesha uthibitisho wa maombi ya kujisajili kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya Ndani.

---

Makampuni yenye nia na uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizotajwa hao juu yanapaswa kuonesha nia yao kwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwenda **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb). Maombi yatumwe kabla au saa **11:00 jioni** kwa saa za Afrika Mashariki (EAT), kabla au tarehe ya **14/12/2024**. Kichwa cha Barua pepe kiwe **REQ-00000659 – Utoaji Msaada wa Huduma ya Manunuzi, Ugavi na Usafirishaji wa Vipuri vya matengenezo, na vifaa vingine vya matumizi ya awali kwa ajili ya EACOP.** Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.**Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza.**

---

**Muhimu**: Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia kulingana na EOI hii na kisha kufanya tathmini kwa kutumia vigezo vya ndani ili kubaini makampuni yatakayojumuishwa kwenye orodha ya (Makampuni) ya awali yaliyokidhi vigezo. Makampuni yaliyofuzu hatua za awali pekee ndiyo yatakayopewa mwaliko wa zabuni, kwa kutia saini Mkataba wa Kutunza Siri (NDA), kama mwendelezo wa wito wa mchakato wa utoaji wa zabuni. Kampuni ya EACOP LTD inayo haki ya kufanya maamuzi yake ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Janga dawa za kulevya linaathiri vijana

**MATUMIZI** ya dawa za kulevya hasa kwa vijana yameathiri nguvu kazi na kusababisha wengi wao kuishia mitaani na kufanya vitendo vya uporaji ili wapate pesa ya kununulia dawa hizo.

Wazazi wamekuwa katika wakati mgumu hasa baada ya kuwasomesha vijana wao, lakini kinyume na walivyotarajia kuwa watakuwa msaada, wamegeuka kuwa mzigo kwa familia.

Wengi wa vijana hao wanaharibika kutokana na makundi wanayoambatana nao na kupata vishawishi vya kutumia dawa hizo.

Baadhi ya wazazi wanatumia gharama kubwa kuwasomesha watoto wao nje nchi, lakini wakirudi nchini tayari wamesha athirika na madawa ya kulevya.

Kutokana na tatizo hilo, serikali imeamua kuchukua hatua ili kudhibiti kikamilifu matumizi ya dawa ya kulevya nchini, kwa kupanga kuhamishia elimu inayoendelea kutolewa katika maeneo mbalimbali, kuipeleka kwenye shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu kama ilivyo kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiwa jijini Mwanza katika kilele cha maadhimisho ya kitaifa ya kupiga vita dawa za kulevya duniani alisema; "ni lazima tuimarishe mikakati yetu ya kukabiliana na mapambano haya na Serikali imejikita katika kutoa elimu ili jamii ifahamu, na tutakwenda kuanzisha klabu katika shule za Msingi, Sekondari mpaka Vyuo Vikuu kama walivyofanya TAKUKURU ili kupunguza kama si kumaliza kabisa tatizo hili."

Pia, vijana wa kitanzania wametakiwa kuachana na matumizi na biashara ya dawa za kulevya na badala yake waungane katika kufanya shughuli halali za kiuchumi ili wajiletee maendeleo katika ngazi ya familia, jamii na hata taifa.

Kadhalika, jamii inatakiwa kuelimishwa zaidi kuhusu athari za matumizi ya dawa hizo na kuwa njia hiyo itakuwa mwarobaini wa tatizo hilo sugu pamoja na kuwawezesha waliotoka kwenye uraibu (waraibu) ili waweze kujumuika na wenzao wafanye kazi na waweze kujisimamia.

Kuhusu taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Said Mtanda, ya hali ya dawa za kulevya katika Mkoa wa Mwanza kuanzia mwaka 2018 hadi 2023, wananchi waliopatikana na bangi ni 1797, mirungi 294, dawa za kulevya (cocaine, heroine na nyingine) 51 na kufanya jumla ya dawa zote kuwa 2142.

Takwimu hizi zinabainisha kwamba biashara na matumizi ya dawa za kulevya mkoani Mwanza ni kubwa na inahitaji msukumo mkubwa kutoka kwa serikali pamoja na wadau mbalimbali ili kuendelea kupambana na wazalishaji, wasambazaji na watumiaji wa dawa hizo.

Ukiangalia vijana wengi wanaoathirika ni kutoka katika majiji ambako hufanyika mambo mengi ya starehe na hupata vishawishi vya kujiingiza kwenye matumizi hayo kama sehemu ya starehe.

Vijana wanao athirika ni wa jinsi zote na kusababisha wazazi wengine kupata msongo wa mawazo kutokana na hali wanayopitia kwasababu wengine hugeuka wezi kwenye nyumba zao ili wapate pesa za kuwawezesha kununua dawa hizo.

Vita ya kupambana na dawa za kulevya ni kubwa kwasababu inahusisha wafanyabiashara wakubwa wenye uwezo kipesa ambao wanaweza kutumia nguvu yao ya pesa kuendeleza biashara hiyo.

Jambo la muhimu kabisa ni elimu kwa vijana hasa katika shule ambako wengi hushawishiwa kutokana na uelewa wao mdogo wa kufahamu lipi zuri na lipi baya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Inasikitisha! Ila niwe wazi, mama kubobea bangi vita inahitajika

**MAMLAKA** ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), inasema imebaini ongezeko kubwa la wanawake wanaojihusisha na uvutaji bangi, kutokana na sababu mbalimbali.

Katika sababu zinazotajwa wavute bhangi hizo, hasa inayotajwa kwa jina la 'skanka', ni migogoro ya kimapenzi, msongo wa mawazo na kutumika kama starehe.

Kamishna Jenerali wa Mamlaka hiyo, Aretas Lyimo anasema hayo wakati akiwasilisha taarifa ya operesheni ya kusaka dawa za kulevya iliyofanyika nchi nzima kati ya Oktoba na Novemba mwaka huu.

Aidha, Kamishna Lyimo anasema 'skanka' ni aina ya bhangi yenye kiwango kikubwa cha sumu ambayo husababisha madhara zaidi kiafya kwa watu ambao wanaitumia.

Nimeelezea kifupi kile ambacho kinasemwa na mamlaka hiyo, jinsi inavyopambana kuhakikisha afya za Watanzania zinakuwa salama kwa kuepuka matumizi ya dawa za kulevya ikiwamo bhangi

Wataalamu wa afya wanabainisha kuwa, mara nyingi wavutaji bangi huvuta moshi kwa nguvu ndani ya mapafu na kuushikilia kwa muda mrefu, ukilinganisha na anayevuta sigara.

Ndiyo staili ya ushuhuda, ila sababu za kimawanazo watumiaji. Niseme, uvutaji unatajwa kitaalamu unasababisha madhara makubwa katika mapafu ya mvutaji.

Hapo ni Mbali na kero ya kama kukohoa na koo kuwasha na kwamba ni uvutaji moshi unaomweka mvutaji katika hatari mara tano zaidi ya kupata saratani ukilinganisha na mvutaji sigara wa kawaida.

Vilevile, wanaeleza kuwa kuna matatizo ya ubongo yanayosababisha kuathiri afya ya akili ni ugonjwa mbaya uwapatao wavutaji wa bangi, na kwamba anayevuta bhangi huwa na uwezo mdogo wa kumbukumbu.

Mbali na hayo, inaelezwa kuwa uvutaji wa dawa hizo humuondolea mtu uwezo wa asili wa kufanya maamuzi sahihi ukilinganisha na mtu ambaye hajihusishi na matumizi ya bangi.

Katika mwendelezo wa maelezo yao, wanasema mtumiaji anapovuta msokoto wa bangi, huanza kufanya kazi baada ya dakika chache na yeye huanza kuhisi mapigo ya moyo yakienda mbio.

Mvutaji pia huanza kubadilika na kuona vitu visivyo katika uhalisia kutokana na maruweruwe na kwamba hayo ni matokeo ya muda mfupi baada kuvuta moshi wa bangi.

Kwa madhara hayo, ingekuwa ni vyema kama wanaovuta skanka kwa lengo la kuondoa msongo wa mawazo, migogoro ya kimapenzi au kutumia kwa starehe wakatafuta vitu vingine visivyo na madhara kiafya.

Mtindo wa kutumia dawa za kulevya kama njia ya kuondoa msongo wa mawazo ni kuhatarisha afya, pia mtindo wa kutumia dawa hizo kama njia ya starehe, vyote ni hatari hivyo wangetafuta starehe nyingine.

Nadhani si vibaya mtu mwenye msongo wa mawazo au migogoro ya kimapenzi akawaona washauri nasaha au wataalamu wa saikolojia ili waweze kumweka sawa kutumia njia ya kuangamiza afya.

Hao wana uwezo wa kumweka sawa mtu mwenye matatizo hayo, sio kutegemea dawa za kulevya, ambazo kimsingi ni hatari kwa watumiaji na pia zinaweza kuwaweka matatani wanapobainika.

Wale wanaotumia dawa hizo kwa ajili ya starehe, ni vyema nao wakatumia vitu ambavyo havina madhara kiafya, kwa sababu kuvuta bangi sio starehe bali ni majanga makubwa.

Uko mitaani, bangi ina majina mengi ambayo watumiaji wake wameipa yakiwamo ya nyasi, majani, mche, ganja, magugu, kitu, sigara kubwa na mengine mengi yanayolenga kushawishi watu kuivuta.

Pamoja na kupewa majina hayo kama njia ya kuipamba, ni vyema jamii ikajua kuwa bangi ni dawa ya kulevya ambayo inatakiwa kuogopwa kwa sababu ni hatari kiafya kwa wanaoitumia.

HABARI KITAIFA

# Wagonjwa 1,000 wapatiwa matibabu ya macho

**Na Kulwa Mzee**

ZAIDI ya wagonjwa 1,000 wa macho na wengine 200 wa rufani, wamepimwa macho na kupatiwa matibabu katika kambi tatu tofauti jijini Dar es Salaam.

Huduma hiyo inaratibiwa na Hospitali ya CCBRT ikiwa ni utekelezaji wa mpango mkakati wa hospitali hiyo kama sehemu ya kuunga mkono juhudi za serikali za kusogeza huduma za jamii karibu na wananchi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana wakati maandalizi ya kambi ya upimaji macho kwenye shule za msingi za Mzambarauni na Amani, Ukonga jijini Dar es Salaam, Dk Sunguro Chacha alisema mwitikio wa wananchi umekuwa mkubwa sana.

"Upimaji macho kupitia kambi hiyo umekuwa na mafanikio makubwa kwani tumebaini wagonjwa wengi wenye matatizo na kuwapa matibabu, ushauri na wengi kuwapa rufani ya matibabu zaidi kwenye hospitali yetu iliyoko Msasani," alisema.

Dk. Chacha alisema kambi hiyo ya siku tatu imeandaliwa kwa ushirikiano kati ya CCBRT na shirika linalohusika na huduma za macho la Light for The World (LFTW).

Mratibu wa Kambi hizo kutoka CCBRT, Mariam Mchomvu, alisema uhamasishaji mkubwa umefanywa na unaendelea mitaani ili wananchi zaidi wenye matatizo ya macho wajitokeze kupima afya kubaini tatizo mapema na kupata matibabu.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Benjamin Mkapa, Deo Joseph, mbali kuishuru CCBRT, aliipongeza pia kwa kutafsiri kwa vitendo 4R za Rais Samia Suluhu Hassan na kuendelea kuifanya shule yake kuwa kambi ya kudumu ya upimaji macho.

"Hii ni mara ya pili shule yangu kufanywa kambi ya upimaji macho na watoto wangu ni wanufaika wa kwanza wa huduma hii. Huduma imekuwa na faida kubwa si kwa watoto pekee bali pia kwa jamii nzima inayotuzunguka," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi waliojitokeza kupima macho, Said Mwakifwamba, mfanyabiashara wa matunda Kariakoo, aliishukuru CCBRT kwa kutoa huduma ya upimaji macho bure na matibabu kwa waliobainika kuwa na matatizo.



Makamu Mkuu wa Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Apolinary Kamuhabwa (wa pili kulia) na Balozi wa Sweden nchini, Charlotte Macia ( katikati) wakibadilishana mkataba baada ya kusainiwa ushirikiano wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 12.5 kati ya nchi hiyo na chuo hicho katika hafla iliyofanyika Dar es Salaam jana. Kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo hicho, Prof. Harrison Mwakyembe na Mshauri wa masuala ya utafiti wa ubalozi huo, Eva Ohlsson. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Mkutano CHADEMA walalamikiwa kugubikwa rushwa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUTANO Mkuu wa uchaguzi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Mkoa wa Singida umelalamikiwa kugubikwa na vitendo vya rushwa kwa baadhi ya wagombea kudaiwa kuwasafirisha, kuwalisha na kuwalaza kwenye nyumba za kulala wageni wajumbe wa mkutano huo.

Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Singida, Jackson Jingu, alitoa malalamiko hayo juzi kwa Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Taifa, Tundu Lissu, ambaye alikuwa anasimamia uchaguzi wa viongozi wa ngazi ya mkoa.

"Makamu Mwenyekiti kuna watu wametoka Ikungi wamekuja kulala hapa Singida ambako ni umbali wa kilometa 45 tu na kwa gari ni mwendo wa nusu saa kufika Singida mjini, lakini wamelala hapa, hatujui walikuja kufanya nini na wameacha kulala huko wakaja hapa Singida, nani aliyewalipia gesti wakalala, nani aliyewalipia chakula wakala," alihoji.

Jingu alisema kwakuwa Singida ndio katikati ya nchi, taifa linaweza kupona kupitia katikati ya nchi kwa kukemea vitendo vya rushwa ambavyo vimekuwa vikijitokeza wakati wa uchaguzi ukiwamo wa ndani ya chama.

Naye Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Lissu alisema rushwa ni adui wa haki na wananchi wamekuwa wakiambiwa tangu wakiwa kwenye matumbo ya mama zao na hata kitabu cha dini Biblia takatifu imeandika rushwa hupofusha macho ya wenye haki.

"Macho ya wenye haki yakipofushwa mtakuwa salama, mtu anayekupa rushwa je anakutakia mema, anaitakia mema nchi hii, anawatakia mema wananchi, kwenye mapambano ya sasa na yajayo atakuwapo au atasimama katika upande wa waliompa asali," alihoji.

Alisema CHADEMA kipo tofauti na vyama vingine kwa kuwa siku zote kimejipambanua kwamba ni chama kinachopinga vita ufisadi hadharani na si kitendo kizuri rushwa kutawala ndani ya uchaguzi wa chama.

"Katika katiba yetu, mwongozo wa chama dhidi ya rushwa toleo la 2002 inaeleza, rushwa kwenye uchaguzi ndani ya chama ni marufuku kwa mwanachama au kiongozi kujihusisha, moja kutoa fedha kwa njia yoyote ile, vyakula vinywaji kwa wajumbe kwa lengo la kupigiwa kura," alisema.


Mkuu wa operesheni Kanda ya Kati, Patrick Ole Sosopi, alisema viongozi waliochaguliwa kuanzia ngazi ya chini hadi juu wafanye kwa kukitumikia chama na sio chama kiwatumikie wao.

"Watanzania wameichoka CCM, wanahitaji kuona viongozi walio imara wa CHADEMA wanaoweza kujenga hoja kuleta matumaini kwa Watanzania ili waweze kufanya maamuzi katika uchaguzi wa serikali za mitaa, mnaona mizengwe mingi katika uchaguzi wa serikali za mitaa ni kwasababu yapo maeneo kuna viongozi wameshindwa kuwajibika," alisema na kuongeza...

"Viongozi wanaishi katika kitongoji, lakini kitongoji kinakosa mgombea na wewe ni mwenyekiti wa mkoa, wapo viongozi kijiji kinakosa mgombea na wewe ni kiongozi wa wilaya au wa mkoa una sababu gani za kubakia kuwa kiongozi wakati unashindwa kusimamia chama kupata wagombea hii hatutakubali," alisema.

Sosopi alisema CCM inapata nafasi sababu yapo maeneo mengi viongozi wa CHADEMA hawatekelezi wajibu wao ipasavyo.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# EWURA yawataka wahitimu uhandisi kutoa huduma bora

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) imewataka wahitimu wa taaluma ya uhandisi wa maji, waitumie taaluma hiyo kuwasaidia wananchi kupata huduma bora ya maji.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mhandisi Mwandamizi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa EWURA, David Linda, baada ya kukabidhi Shilingi milioni sita pamoja na kompyuta mpakato kwa wanafunzi wawili wa chuo cha maji waliofanya vizuri katika kozi ya Uhandisi katika sekta ya maji na usafi wa mazingira.

Linda alisema bado wanahitaji wataalam ambao watatumia vizuri taaluma yao kutoa huduma bora kwa Watanzania.

"Tunatambua umuhimu wa elimu na zaidi sana kwenye sekta ya maji, tunaona upo umuhimu wa kuwapa motisha vijana ili wafanye vizuri sana katika taaluma hii," alisema Linda.

"Kwa hiyo tumetoa zawadi kwa wanafunzi bora ambao wamefanya vizuri kwenye eneo la maji, usafi wa mazingira na eneo la ubora wa maji, tumefanya hivyo kwa sababu ya umuhimu wake ili vijana waliopo katika eneo hilo wafanye vizuri zaidi, lengo ni kutaka sekta hii ifanye vizuri zaidi, tupate wataalam ambao wataisukuma kwenda mbele.

> **"Sasa hatuwezi kupata kama hatuna wataalam kwenye hilo eneo, hivyo lengo letu kuweka motisha ni kuwaambia wataalam ongezeni nguvu, pambaneni tupate bidhaa ambayo tunaihitaji kwenye...**

Alisema lengo la dunia ni kuhakikisha kila mtu anapata majisafi na salama.

"Sasa hatuwezi kupata kama hatuna wataalam kwenye hilo eneo, hivyo lengo letu kuweka motisha ni kuwaambia wataalam ongezeni nguvu, pambaneni tupate bidhaa ambayo tunaihitaji kwenye sekta ya maji," alisema Linda.

"Tuna imani wanavyokuja mitaani kuanza kuwahudumia Watanzania na EWURA kama Mdhibiti Nishati na Maji ambayo kiukweli lengo kuu ni kuhakikisha inatoa huduma bora, tunataka mteja apate majisafi na salama, lakini pia yamfikie kwa wakati."

Alisema huduma wanayotakiwa kupatiwa wananchi ni wanapoihitaji wanaipata kwa wakati na kwa ubora.

"Meseji kubwa hapa ya sisi kufanya hivi ni kuwaambia kwamba tunawahitaji huku kile ambacho wamekipata huko chuoni waje wakifanyie kazi huku kuwahudumia Watanzania, zaidi watambue sekta hii kuna udhibiti, kwamba huduma zinazotolewa zinazingatia viwango ambavyo vimewekwa na Serikali ya Tanzania na dunia.

"Lakini hao wataalam wanapokuwa wanatoa hizo huduma, bado pia tuna nafasi ya kuangalia, kuwaangalia, kwa sababu huduma ni lazima iwe endelevu," alisema Linda.

Emmanuel Mnyaki, mwanafunzi bora katika kozi ya Uhandisi wa Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira, alisema ili kufanya vizuri katika eneo hilo ni lazima mwanafunzi akubali kusoma kwa bidii na kuweka kando mambo mengine.

"Nilipata wazazi ambao wamenisapoti na nimepambana sana kusoma kwa bidii, niliamua kuacha mambo mengine mengi yasiyo ya msingi ili nipate muda wa kutosha kusoma," alisema Mnyaki. Florence Theonist, mhitimu wa kozi ya Uhandisi wa Maji na Usafi wa Mazingira, alisema siri pekee ya mwanafunzi kufanya vizuri katika eneo hilo ni kusoma kwa bidii.

"Kwa hiyo nimefarijika sana kuona EWURA wamethamini kile ambacho tumekifanya, hili ni somo kwa wanafunzi wengine kujituma ili wafanye vizuri kwenye masomo yao," alisema Theonist.



Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA), Dk. Stella Bitanyi (kushoto), akitoa maelezo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Viwanda Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu taratibu za uzalishaji wa chanjo unaofanywa na Taasisi ya Chanjo Tanzania (TVI), walipotembelea Taasisi hiyo kukagua maendeleo ya uzalishaji wa chanjo za mifugo. Wa pili kutoka kushoto ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Viwanda Biashara, Kilimo na Mifugo, Deodatus Mwanyika na wa pili kutoka kulia ni Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## TVLA yapongezwa kuzalisha chanjo ya mifugo

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo chini ya Mwenyekiti, Deodatus Mwanyika imeipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) kwa uzalishaji wa chanjo za mifugo ambazo zinatumika kuboresha afya za mifugo hiyo nchini.

Mwanyika kwa niaba ya kamati hiyo walitembelea Taasisi ya Chanjo Tanzania (TVI) iliyopo Kibaha, Mkoa wa Pwani Novemba 12, 2024.

Naibu waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti, alisema mipango ya wizara ni kuendelea kuhamasisha pamoja na kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu umuhimu wa kuchanja mifugo.

Aidha, Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA), Dk. Stella Bitanyi, alisema kwa sasa wameanza kuwafikia wafugaji moja kwa moja kuwapa elimu ya umuhimu wa chanjo kwa mifugo yao.

Taasisi ya Chanjo Tanzania (TVI) ipo chini ya TVLA na jukumu lake kubwa ni kufanya utafiti na kuzalisha chanjo.

# Verma ateuliwa balozi nchini Liberia

**Na Romana Mallya**

BALOZI mdogo wa India nchini, Manoj Verma ameteuliwa kuwa Balozi wa Liberia na anatarajia kuanza kazi yake mpya hivi karibuni.

Verma ameshiriki kwa kiasi kikubwa kuratibu ziara ya kihistoria ya Rais Samia Suluhu Hassan nchini India iliyofanyika mwezi Oktoba, 2023.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje ya India, ziara hiyo ilileta uhusiano wa pande mbili kuwa na ushirikiano wa kimkakati na kutangazwa kwa mipango mingi ya kuimarisha kushirikiana katika elimu, biashara na maendeleo.

Taarifa hiyo ilisema kabla ya kuteuliwa Tanzania, alifanya kazi katika Idara ya Ushirikiano wa Maendeleo, akilenga kukuza mipango ya ushirikiano ya India nje ya nchi. Ilisema tangu aanze huduma yake Tanzania mwezi Desemba 2021, ameleta mchango mkubwa katika kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia kati ya India na Tanzania.

"Katika mwaka wa fedha 2023/24 (Aprili na Machi, mwaka huu) biashara kati ya nchi hizo mbili ilifikia Dola za Kimarekani bilioni 7.9 na kufanya Tanzania kuwa mshirika wa pili mkubwa wa biashara wa India barani Afrika.

Kadhalika, taarifa hiyo ilitaja moja ya mafanikio makubwa aliyofanya ni kuratibu shughuli za kuanzishwa kwa Kampasi ya IIT Madras katika visiwa vya Zanzibar (IITMZ), kampasi ya kwanza ya Taasisi ya Teknolojia ya India (IIT) barani Afrika.

"IITMZ ilizinduliwa mwezi Novemba, 2023 na Rais Hussein Ali Mwinyi wa Zanzibar na tangu wakati huo imeshafanya udahili wa wanafunzi kwa awamu ya pili

"Kampasi hii inatarajiwa kuwa chachu ya mabadiliko katika elimu ya juu ya Tanzania, kutoa mafunzo ya uhandisi ya kiwango cha dunia na kukuza ubunifu," alisema.

Taarifa hiyo ilisema Verma anakwenda nchini Liberia akiwa na uzoefu mkubwa wa zaidi ya miaka 25 kidiplomasia akihudumu katika nchi za Saudi Arabia, Urusi, Marekani, Sudan na Mali.

Taarifa hiyo ilisema kuwa pia, ametoa mchango muhimu katika Makao Makuu ya Wizara ya Mambo ya Nje huko New Delhi.

"Kazi alizowahi kuzifanya ni pamoja na majukumu katika Idara ya Umoja wa Mataifa, Idara ya Pakistan-Afghanistan-Iran (PAI) na Idara ya Utawala.

Kadhalika, taarifa hiyo ilisema, Verma anakwenda nchini Liberia kuchukua nafasi ya balozi wakati ambapo kuna ukuaji mkubwa katika uhusiano kati ya Liberia na India.

Ilisema uzoefu wake katika maeneo mbalimbali unatarajiwa kusaidia kuhamasisha biashara, uwekezaji na uhusiano wa kitamaduni kati ya nchi hizo, hasa wakati ambapo zinaangazia fursa mpya za ushirikiano katika kilimo, afya na elimu.





# TAKUKURU yaibua madudu miradi ya maendeleo

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani hapa imebaini mapungufu kwenye miradi mitano ya maendeleo yenye thamani ya zaidi ya Shilingi milioni 500 na kuchukua hatua.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Mkuu wa TAKUKURU wa mkoa huo, Noel Mseo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusiana na ufuatiliaji wa miradi 33 kwa kipindi cha miezi mitatu.

Alitaja miradi hiyo kuwa ni ya sekta za elimu, afya, barabara, mifugo, maji na ujenzi wa nyumba za watumishi.

"Miradi yote ilikuwa na thamani ya Sh. Bilioni 5.4. Katika ufuatiliaji huo, mitano yenye thamani ya Sh. milioni 579,395,980 ilibainika kuwa na mapungufu na hatua mbalimbali zilichukuliwa ili kurekebisha mapungufu hayo," alisema Mseo.

Alitoa rai kwa wananchi katika maeneo miradi hiyo inatekelezwa kuwa makini na kufuatilia kwa kuwa ushiriki wao ni muhimu kuhakikisha inakamilika kwa wakati.


**"Miradi yote ilikuwa na thamani ya Sh. Bilioni 5.4. Katika ufuatiliaji huo, mitano yenye thamani ya Sh. milioni 579,395,980 ilibainika kuwa na mapungufu na hatua...**

Mseo aliwakumbusha wakandarasi, wazabuni, wahandisi, mafundi na wanakamati kutimiza wajibu wao na kutunza nyaraka za matumizi ya fedha.

Mseo alisema katika kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa wamejipanga kudhibiti vitendo vya rushwa kwa kushirikiana na wananchi, vyama vya siasa na wadau.

"Niwaombe wananchi wote kutoa taarifa kwetu pale wanapoona viashiria vyovyote vya rushwa katika maeneo yao wakati wa mchakato wa kuwapata viongozi watakaogombea," alisema Mseo.

Baadhi ya wakazi wa mjini Njombe, akiwemo Kaini Nyingu, alisema vitendo vya rushwa katika taasisi za umma havipaswi kupewa nafasi wakati wa utoaji huduma kwa wananchi.



Diwani wa kata ya Bwembwera wilayani Muheza Tanga, Ally Nyangasa juzi akiwasilisha taarifa yake ya kata katika mkutano wa baraza la madiwani la kuwasilisha taarifa za kata katika ukumbi wa Tate Plus.
**PICHA: STEVEN WILLIAM**

# SIDO yaagizwa kukopesha vyuo vya ufundi

**Na Renatha Msungu,**
IRINGA

SERIKALI imeliagiza Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) kutoa mikopo kwenye vyuo vya ufundi nchini kuendeleza teknolojia ya ubunifu itakayotumiwa na wahitimu kujiajiri.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe alitoa agizo hilo wakati wa mahafali ya tisa ya Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi cha RDO Mdabulo yaliyofanyika jana katika viwanja vya chuo hicho kilichopo wilayani Mufindi Mkoa wa Iringa.

Kigahe, alisema ameridhishwa na bidhaa zinazotengenezwa na wanafunzi wa chuo hicho kupitia teknolojia na kwamba wakipewa mikopo midogo na SIDO watazidi kupanua wigo wa ubunifu na kuinua uchumi wao.

"Nawapongeza sana wanafunzi wa chuo hiki na wakufunzi wao kwa kubuni teknolojia hiyo, jitihada zaidi zinahitajika kutoka kwa wakufunzi wao ili wapige hatua kwa hiki wanachofanya," alisema.

Alisema ubunifu huo na elimu ya ujuzi wanayopata kutoka chuoni hapo itawasaidia kujiajiri badala ya kusubiri kuajiriwa.

Alisema baada ya kupata maelekezo kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan kuanzisha vyuo vya ufundi stadi kila wilaya, wao kama wizara wataendelea kushirikiana nao kuhakikisha jamii inanufaika nayo kwa kujiajiri.

Alikipongeza RDO Mdabulo kutokana na fani za ufundi wanazotoa kwa wanafunzi na anaamini zinakwenda kuwasaidia kujiajiri baada ya kuhitimu masomo yao.

Vilevile, Kigae aliwataka wahitimu kwenda kutumia ujuzi waliopata chuoni hapo kujiajiri badala ya kusubiri kuajiriwa. Katika risala ya wahitimu hao wa mwaka wa tatu iliyosomwa na Jackline Kibuga, waliiiomba serikali kusaidia kuelimisha jamii umuhimu wa elimu ya ufundi stadi na kutoa kipaumbele kwa wahitimu wake.

Pia waliiomba serikali kuwaunganisha na viwanda ili kupata ajira na kuendeleza ujuzi wao.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Maendeleo Vijijini (RDO), Fidelis Filipatali, aliishukuru serikali na wadau wao kwa kuhakikisha shirika hilo linapiga hatua katika kuisaidia jamii.

Filipatali, alisema lengo lao ni kuona jamii inanufaika na shirika hilo kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya elimu, maji na afya.

# Serikali yapongeza kuwatimua wanaotoa elimu kwa mtandao

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

BAADHI ya wakazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma wameipongeza serikali wilayani hapa kwa kuwatimua baadhi ya watu waliokuwa wakiendesha biashara haramu ya kutoa elimu kwa njia ya mitandao bila ya kuwa na vibali na leseni.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na Nipashe juzi mjini hapa, wakazi hao, walisema kwa muda mrefu liliibuka kundi la watu na kuanzia vyuo vya kutoa mafunzo ya kutafuta masoko kwa mitandao hiyo.

Walisema mafunzo hayo yalikuwa yanatolewa katika maeneo ya Mjimwema na Msamala kwa vijana kutoka ndani na nje ya nchi.

Said Omar, Mkazi wa Mjimwema, alisema hatua iliyochukuliwa na uongozi wa wilaya hiyo kupiga marufuku vyuo hivyo na watu hao kutimuliwa inastahili kupongezwa kwa kuondoa mazingira ya utapeli kwa vijana.

Alisema vijana hao walikuwa wakishawishiwa kuwasiliana na ndugu zao wawatumie fedha za mtaji kuanzisha biashara wanazofundishwa kuzifanya kwa mtandao.

Khalfan Msoa, alisema vijana wamekuwa wakidanganyika kuwa elimu hiyo inayotolewa na vyuo hivyo itawasaidia kuondokana na umaskini na kujikuta wakiishi katika mazingira magumu zaidi baada ya kutapeliwa fedha.

Mkufunzi Msaidizi wa Chuo cha Alliance in Motion Global, Jovitha Lubida, alisema kwa muda mrefu wanaendesha mafunzo sehemu mbalimbali nchini ya kuwajengea uwezo vijana kujiajiri.


Kiongozi Mkufunzi wa QNET, Yona Maganga, alisema chuo hicho kipo kisheria na kinaendesha mafunzo kwa kufuata taratibu zilizopangwa na Wizara ya Elimu kutoa elimu kwa njia ya mtandao.

Diwani wa Mjimwema, Sylvester Mhagama, alisema katika kata yake, watu waliokuwa wakijihusisha na biashara hiyo waliondolewa, lakini anashangaa baada ya kuona baadhi wamerudi kuendesha mafunzo kwa vijana ambayo ni batili.

Mkuu wa Wilaya ya Songea, Wilman Kapenjama na kamati yake ya ulinzi na usalama walikwenda kwenye maeneo ambayo mafunzo hayo yanatolewa na kubaini vyuo hivyo vipo tangu mwishoni mwa mwaka jana.

Alisema amechukua uamuzi wa kuviondoa vyuo hivyo kwenye wilaya yake mpaka wamiliki wake wafuate taratibu za kisheria

Kapenjama alifafanua kuwa vyuo hivyo vinachukua vijana ndani na nje ya nchi baada ya kudanganywa kuwa kuna ajira na wakifika Songea wanalazimishwa kutoa fedha kuanzia Sh. 100,000 hadi 600,000 kila mmoja.





# Bibi anyweshwa pombe, alawitiwa, abakwa

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mwanza linamshikilia Dalali Atanas Masubo (65), Mkazi wa Mtaa wa Kashishi Kata ya Nyamhongolo Wilaya ya Ilemela kwa tuhuma za kumlawiti na kumbaka bibi mwenye umri wa miaka 68 baada ya kumnywesha pombe kali.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Wilibroad Mutafungwa alithibitisha kutokea kwa tukio hilo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana.

Alisema mtuhumiwa huyo anadaiwa kufanya unyama huo dhidi ya mwanamke huyo, ambaye ni jirani yake Novemba 7, mwaka huu majira ya saa 7:00 mchana nyumbani kwake.

Mutafungwa alisema baada ya bibi huyo kufika nyumbani mtuhumiwa huyo ambaye ni jirani yake, alimkuta akinywa pombe na kumkaribisha na kupata pamoja kilevi hicho.

**Mutafungwa alisema baada ya bibi huyo kufika nyumbani mtuhumiwa huyo ambaye ni jirani yake, alimkuta akinywa pombe na kumkaribisha na kupata pamoja kilevi hicho.**

"Wakiwa wanaendelea kunywa pombe ndipo Masabo alimuagiza binti wa kazi kwenda kununua pombe nyingine ili waendelee kunywa, ndipo alipata mwanya wa kumuingilia bibi huyo kimwili huku akimtishia kumuua kwa kumcharanga kwa panga alilokuwa ameshika mkononi," alisema.

Alisema baada ya tukio hilo, bibi huyo alifanikiwa kukimbia na kutoa taarifa polisi na kuanza uchunguzi mara moja. "Amekamatwa (mtuhumiwa) na kuhojiwa kuhusiana na tukio hilo la kikatili," alisema.

Kwa mujibu wa Kamanda huyo, uchunguzi wa polisi umekamilika na jalada limepelekwa ofisi ya mashtaka kwa hatua zaidi za kisheria. Akizungumzia tukio jingine, Kamanda Mutafungwa amesema wanawashikilia watu 90 kwa tuhuma mbalimbali za makosa ya jinai.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa katika msako uliofanywa na askari wa jeshi huo Novemba 12, mwaka huu usiku katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

Alisema kati ya hao 42 ni vijana wanaoishi mitaani kwa tuhuma za kuwapora baadhi ya wakazi wa jiji hilo fedha na mali kisha kutumia kucheza kamari.

"Watuhumiwa wengine 48 kati yao wanawake 34, wamekamatwa kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya ukahaba na matumizi ya dawa za kulevya," alisema.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, Mibako Mabubu akizungumza na madiwani na watumishi wa halmashauri hiyo wakati wa kikao cha baraza la madiwani cha robo ya kwanza yam waka wa fedha 2024/2025, kulia kwake ni Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo Rose Manumbu, kushoto ni Katibu Tawala wa mkoa wa Shinyanga, Salumu Hamduni, Katibu tawala msaidizi Ibarahim Kamanda, jana. **PICHA; SHABAN NJIA.**

# Shule stahiki sasa kusajiliwa Buchosa

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Buchosa wilayani hapa Mkoa wa Mwanza, Idama Kibanzi amemtaka Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kutoa usajili kwa shule shikizi baada ya kukidhi vigezo ili zianze kutoa huduma kwa wanafunzi.

Kibanzi alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na Nipashe kuhusiana na kero wanayoipata wanafunzi kutembea umbali mrefu kufuata masomo licha ya kuwepo shule shikizi kwenye maeneo wanayoishi ambazo ujenzi wake umekamilika, lakini hazijasajiliwa na kuanza kutumika. Idama, alisema lengo la kuanzisha shule hizo ni kuwaondolea adha wanafunzi kutembea umbali mrefu kufuata elimu huku wakiwa na umri mdogo.

Alisema shule hizo zinaanzishwa na wananchi kwa kuchangishana fedha.

Alisema anashangaa sababu za Mkurugenzi huyo kushindwa kuzipa usajili na kufunguliwa.

Mkurugenzi Mtendaji huyo, Benson Mihayo alithibitisha kuwapo kwa shule hizo huku baadhi wanafunzi wakiwa wameanza kusoma.

Hata hivyo, Mihayo aliahidi kuhakikisha shule hizo zinapata usajili, kufunguliwa na kupokea wanafunzi.

# Madereva mabasi mikoani wafungiwa leseni

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MADEREVA sita wa mabasi yaendayo mikoani, wamefungiwa leseni kwa kipindi cha miezi mitatu kwa kuhatarisha maisha ya watu wakiwa safarini.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilbroad Mutafungwa alisema kuwa madereva hao walikamatwa katika opereshini iliyofanywa na askari wa kikosi cha usalama barabarani mkoani hapa dhidi ya madereva wa mabasi ya mabasi hayo wanaokiuka sheria na kuhatarisha maisha ya abiria na watu wengine.

Mutafungwa alisema madereva wengine walikamatwa kwa kuendesha gari kwa njia ya hatari na kuyapita magari mengine sehemu iliyokatazwa bila kuchukua tahadhari. Wengine ni kuendesha bila ya kujali watumiaji wengine wa barabara kwenye eneo lenye mkusanyiko mkubwa wa watu, kuyapita magari mengine sehemu isiyoruhusiwa kwenye makazi ya wattu, mwendo kasi na kuzidisha abiria.

Kwa mujibu wa Mutafungwa, madereva hao wametakiwa warudi vyuoni kwa mafunzo zaidi.

# Kicheko TASAF kubadili maisha yao

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

ANNA Makonda, Mkazi wa Kata ya Ndala Manispaa ya Shinyanga ameusifia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwa kumuondoa katika ufukara uliokithiri wa kula mlo mmoja na kuishi katika nyumba ya udongo.

Anna alibainisha hayo juzi akizungumza na Nipashe kuhusu mafanikio aliyopata kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini wa TASAFkwa kumwezesha kuishi maisha bora zaidi, kusomesha watoto, wajukuu zake na kujenga nyumba ya kisasa.

Yeye na wanufaika wengine, walibainisha mafanikio yao juzi wakati waandishi wa habari na maofisa wa TASAF walipotembea kaya zao.

Alisema aliingia kwenye mpango huo mwaka 2015 akiwa na maisha hayo na watoto wake saba.

Anna, alisema wakati akiendelea kupokea ruzuku ya TASAF Sh.56,000, alijiunga kwenye kikundi cha akiba na mikopo, baada ya kuvunjwa, alipata Sh. 800,000, akanunua nguruwe watatu, aliwazalisha wakafika wanane, akawauza baadhi na kuanza ujenzi wa nyumba ya kisasa.

Alisema kwa sasa hali yake ya maisha ni nzuri kwa sababu siyo maskini tena na kwamba ametoka kwenye mpango huo na kuachia fursa hiyo kwa kaya nyingine maskini ili nazo zinufaike kwa kuinuka kiuchumi.

"Sasa hivi siyo maskini tena, naishi kwenye nyumba ya kisasa, nasomesha watoto wangu hadi wajukuu, nina miliki mifugo nguruwe wanane, bata watano na kuku 10," alisema.

Alitoa wito kwa wenzake ambao bado wapo kwenye mpango huo kutumia fedha vizuri kwa malengo kusudiwa na siyo kutumbua, lasivyo wataendelea kuwa maskini.

Walengwa wengine wa mpango katika Manispaa hiyo nao wameelezea mafanikio waliyopata kwa kuondokana na umaskini na kujenga nyumba za kisasa na kuachana na maisha ya kuendelea kuishi kwenye makazi duni ya udongo.

Kwa mujibu wa Ofisa Ufuatiliaji Mpango huo Wilaya ya Shinyanga, Tabu Maro, alisema walengwa walioondolewa baada ya kuimarika kiuchumi katika Manispaa hiyo ni 1,500, waliosalia 2,600 na Halmashauri ya Wilaya hiyo 2,500 na wanaoendelea 8,200.



Ukurasa 12

**Samia akiwa mwalikwa Jumatatu, fahamu maudhui ya kikao cha G20 na historia yake**




Ukurasa 13

Hebu tuache utani katika mambo makini



Ukurasa 14

**Mkurugenzi Kafulila na darasa la Kituo Ubia inavyotekeleza PPP**


# BUFE

IJUMAA NOVEMBA 15, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


WAZIRI AKIINYOSHEA KIDOLE...

# Wizi madini waumiza kichwa Shinyanga, imejipanga kwa makali ya kisu ikomeshe

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KUNA walakini wa kiutawala, kuhusu utoroshaji madini, mamlaka zote za usimamizi mkoani hapa zikilalamika kuwapo mipenyo yenye athari za moja kwa moja kiuchumi.

Huo ni utoroshaji madini unaofanywa kwa asilimia kubwa na wachimbaji wadogo, wakishirikiana na baadhi ya watumishi wa sekta hiyo.

Jambo hilo linatokea huku tovuti ya Wizara ya Madini inafafanua wachimbaji wadogo wa madini, wamekuwa wakichangia Pato la Taifa katika eneo hilo kwa asilimia 40 kufika mwaka 2023.

Mwaka 2019 serikali kupitia Tume ya Madini, ilianzisha masoko ya madini kwa nchi nzima, hasa kwenye maeneo yanakochimbwa madini, lengo ni kusaidia wachimbaji wadogo kuuza madini kwa urahisi na kupata fedha halali, kuzuia utoroshaji wa madini pamoja na serikali kupata mapato kupitia tozo mbalimbali.

Uchunguzi wa Nipashe umebaini kwamba masoko hayo ya madini katika miaka ya nyuma yalisaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti mianya ya utoroshaji madini, na kuzuia kuwapo mtiririko haramu fedha zake.

Waziri wa Madini, Athony Mavunde akiwa mkoani Tanga Septemba 15 mwaka huu, akifunga Kikao Kazi cha Menejimenti ya Tume ya madini, anasema mkoa wa kimadini Kahama, ndio unaoongoza kwa utoroshaji madini.

Hilo linatolewa ufafanuzi na Ofisa Madini mkazi mkoa huo wa kimadini, Winfrida Mrema, anayekiri utoroshaji madini umekuwa ukisababisha serikali kukosa mapato na watu kujipatia fedha haramu kinyume cha utaratibu.



Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, akionesha fedha Sh.milioni 97 na madini ya dhahabu yenye uzito wa gramu 930.88 yenye thamani ya Sh.milioni 93, zilizokuwa zinatoroshwa na watu Ilogi wilayani Kahama mkoani Shinyanga. **PICHA: MARCO MADUHU**

Anasema, kwa sasa wapo kwenye msako wa kuwakamata wanaojihusisha na utoroshaji huo wa madini, na kuna kundi la waliokamatwa.

Hapo anadokeza kuwapo ofisa mmoja wa madini anayetuhumiwa kushiriki vitendo hivyo na wapo kwenye mikono ya sheria, huku hatua za kikao kisheria zikichukua nafasi.

"Utoroshaji wa madini ni tatizo kubwa kwa serikali kukosa mapato, mfano mwaka 2023 tulipangiwa kukusanya kiasi cha fedha Sh. bilioni 29.75, lakini tukakusanya bilioni 24.9," anasema Winfrida.

Anaeleza kwamba, mwaka huu kiserikali wamepangiwa kukusanya Sh. bilioni 34.6, lakini hadi Septemba wameshakusanya Sh. bilioni 32.12 sawa na asilimia 92.63.

Hapo ofisa huyo anafafanua ni mwenendo mzuri, hasa ikitokana na kuanza kudhibiti mianya ya utoroshaji madini.

**DC KAHAMA**

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita anaeleza hatua walizochukua kudhibiti mianya ya utoroshaji madini, kwa kushirikiana na Tume ya Madini.

Hapo anataja walianza kufanya vikao na wadau wa madini kubaini sababu zinazochangia kukithiri kwa utoroshaji, hasa kwenye machimbo na masoko ya madini.

Anasema baada ya kukaa nao, wadau walitoa hoja na sababu za madini kutoroshwa, ikiwamo madai ya kuwapo tozo nyingi kutoka kwenye halmashauri, na kuwapo upungufu wa masoko ya madini.

Mboni anasema, baada ya masoko mengine kufungwa likiwamo la Segese likabaki moja tu la Kahama Mjini.

"Hoja hizi tulizipokea na tupo kwenye utaratibu wa kuzifanyia kazi na katika kuendelea kudhibiti mianya ya utoroshaji madini.

"Pia tumeimarisha ulinzi zaidi kwenye uwanja wa ndege Kahama, machimboni dhahabu na kwenye masoko ya madini, yani kila sehemu tumeweka watu wetu," anasema Mboni.

Anasema kwamba msako bado unaendelea wa kuwakamata watu ambao wamekuwa wakitorosha madini, na ambao huwakamata wamekuwa wakiwachukulia hatua kali za kisheria na kuwafungia leseni zao.

Mkuu wa Wilaya anasema, msako huo, katika Mgodi wa Mwime wameshawafungia wachimbaji watatu kujihusisha na madini na kwamba katika soko la madini Kahama, wamewafungia pia lesseni zao wafanyabiashara watatu kutokana na kuhusika na utoroshaji huo wa madini.

Anasema, baada ya kudhibiti tatizo hilo la utoroshaji madini kwa kiasi kikubwa, wameanza kuvunja rekodi ya ukusanyaji mapato, ambapo kwa mwezi Julai pekee wamekusanya Sh. bilioni 11, lakini awali walikuwa wakikomea Sh. bilioni 9.

**MRATIBU UWEKEZAJI**

Mratibu wa Uwekezaji mkoani Shinyanga Dotto Maligisa, anasema tatizo la utoroshaji madini Kahama, linasababishwa na jengo la soko la madini kuwa dogo, na hivyo wafanyabiashara wa madini kukosa usiri na kuhofia usalama wao.

**INAENDELEA UK.14**

UCHUMI

## MWANAMAMA MGENI RASMI WA KWANZA...

# Samia akiwa mwalikwa Jumatatu, fahamu maudhui ya kikao cha G20 na historia yake

**Na Mwandishi Wetu**

AKIWA na miezi kadhaa tangu kuingia madarakani, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akahutubia Mjadala Mkuu wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, kwenye makao makuu yake jijini New York, Marekani, ikiwa ni mara ya kwanza tangu ashike wadhifa huo mwezi Machi.

Hapo akawa anamulika masuala mbalimbali kuanzia uchumi, siasa, tabianchi, usawa wa jinsia na janga la Covid - 19 lililokuwa linapamba moto wakati huo.

Rais Samia katika hotuba yake ya kwanza ana kwa ana kwenye mjadala huo, ambayo kiuchumi na kidiplomasia ikafafanuliwa kuwa na maana kubwa na muhimu kwake.

Hapo akaanza na dhana ya ushirikiano wa kimataifa, akitamka katika ujumbe uliotoa mvuto kwa kutamka: "Chini ya uongozi wangu, Tanzania itaendelea kuwa mshirika muhimu wa Umoja wa Mataifa na muungaji mkono wa kutegemewa wa suala la ushirikiano wa kimataifa.

"Tutanyoosha mkono kwa wale wanaotukumbatia na kushirikiana nasi. Tutaendelea kuwa Tanzania ambayo mmeifahamu kwa muda mrefu.

"Tanzania yenye amani na ambayo inashirikiana na chi zote kubwa au ndogo, zenye nguvu au zisizo na nguvu, tajiri au masikini kuifanya dunia dunia yetu kuwa bora kwa ajili yetu sote."

Ushuhuda na mwendelezo wa ahadi ya kwanza na mwendelezo wa utekelezaji wa mialiko, sasa anapata mialiko mingi kimataifa, inayombebesha heshima kimataifa duniani, Jumatau ijayo akitarajiwa kuwapo jijini Rio De Janeiro Brazil, kwa siku mbili.

Huo ni mkutano wa viongozi wa kundi la nchi 20 zinazohimili uchumi wa dunia, mwaliko ukitolewa na Mwenyekiti wao, Rais Luiz Inacio Lula da Silva wa Brazil, huku Dk. Samia akiweka rekodi kuwa Rais wa kwanza mwanamke kuhudhuria mkutano wa viongozi wa kundi hilo, tangu kuitwa G20 mwaka 2009, ikipanda kutoka kundi la nchi nane, G8.

Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, inaonesha kuwa marais wastaafu nchini Benjamin Mkapa na Jakaya Kikwete, walishiriki mikutano ya G8 iliyofanyika mwaka 2005 na 2008.

Kimsingi, kundi la G20 linaundwa na mataifa ya: Argentina, Australia, Brazil, Canada, China, France, Ujerumani, India, Indonesia, Italy, Japan, Jamhuri ya Korea, Mexico, Russia, Saudi Arabia, Afrika Kusini, Uturuki, Uingereza na Marekani.



Ndivyo ilivyokuwa kikao cha G20 nchini India, mwaka jana. **PICHA:MTANDAO**

> **"Safari ya Rais Dk. Samia mwezi huo ikamfikisha Msumbiji, safari hiyo akiwa makao makuu Maputo na ziara ya 2021, alikuwa Pemba kunakoathiriwa na hali ya hewa.**

Pia, kuna wanachama wa kitaasisi; Umoja wa Afrika (AU) na Umoja wa Ulaya (EU), ambao mara nyingi unawakilishwa na rais wake. Vilevile kuna wadau; taasisi zinazowakilishwa na watedaji wake wakuu, ambazo ni: Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF); Benki ya Dunia (WB); pia Kamati ya Maendeleo ya IMF na Benki ya Dunia

Aidha, kimuundo G 20 hufanya kazi bila ya sekretarieti ya kudumu wala wafanyakazi na uenyekiti wake huzunguka kila mwaka, kati ya wanachama na mwenyekiti anatokana na mmoja wa mataifa waasisi.

Mwenyekiti aliyeko, huunda sekretarieti ya muda kwa wakati wake, inayoratibu kazi ya kikundi na inapanga mikutano yake.

Safu hiyo ya uenyekiti tangu chombo hicho kianze, iko ifuatavyo kihistoria ya nchi na msaka husika katika mabano: 2001 ni Ujerumani na kisha Canada mwaka huo; ikiafuata India (2002), Mexico ( 2003), Ujerumani (2004),China (2005), Australia (2006), Ufaransa (2007), Marekani (2008) na Uingereza (2009),

Wengine ni: Korea Kusini (2010), Ufaransa (2011), Mexico (2012), Russia (2013), Russia (2014), Uturuki (2015), China (2016), Ujerumani (2017), Argentina (2018), Japan (2019), Saudi Arabia (2020), Italia (2021), Indonesia (2022) na India mwaka jana.

Pia, Umoja wa Afrika (AU) umejumuishwa kuwa mwanachama wa kudumu katika muungano G20 katika mkutano uliokamilika nchini India mwaka jana na sasa una hadhi sawa na Umoja wa Ulaya (EU).

Viongozi wa mataifa wanachama wa G-20 hukutana kila mwaka mara mbili katika Kongamano la G-20.

G-20 hufanya kazi bila sekretarieti ya kudumu wala wafanyakazi. Uenyekiti huzunguka kila mwaka kati ya wanachama na huchaguliwa kutoka kwa kambi tofauti za nchi.

### MIKUTANO G20

Historia ya Makongamano ya G-20, yalianzishwa ikiwa mwitikio wa tatizo la fedha kati ya mwaka 2007 hadi 2010, pia kuonekana nchi zinazostawi hazikujumuishwa vya kutosha katika majadiliano ya kiuchumi duniani na utawala.

Makongamano ya G-20 ya wakuu wa nchi au serikali yalifanyika mbali na mikutano ya G-20 ya mawaziri wa fedha na magavana wa benki kuu, walioendelea kukutana kuandaa kongamano la wakuu wa nchi, pia kutekeleza maamuzi yao.

### HISTORIA ZIARA ZA SAMIA

Pata historia ya ziara ambazo amefanya Rais tangu kuingia madarakani miaka mitatu na nusu sasa.

Mwaka 2021; Rais Dk. Samia akianzia mwezi Aprili alifanya ziara za kujenga uhusiano katika nchi jirani na hata kushuhudia uchaguzi katika Afrika Mashariki, Uganda, Kenya, Burundi na huko Msumbuiji katika kikao cha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Katika historia hizo, baadhi ya maeneo kama Burundi akifika zaidi ya mara moja na baada ya nusu mwaka kuanzia mwezi Julai, pia akafika nchi za Malawi, Rwanda na Zambia alikohudhuria matukio muhimu.

Baadaye kuanzia mwezi Septemba ya mwaka huo 2021, Rais Dk Samia akafika katika mataifa ya Marekani, Uingereza, Misri na Scotland katika safu yake ya umahiri, kikao cha hali ya hewa duniani.

### MWAKA 2022

Ni mwaka huo akazuru nchi zaidi ya 15 akiwajibikia nchi kiuchumi na diplomasia ya uhusiano mwema, huku akiwa na mvuto uliompatia mialiko mingi kimataifa.

Hapo kunatajwa mataifa kama Msumbiji, Ufaransa, Ubelgiji kwenye kikao cha pamoja cha AU na EU; pia akafika Jamhuri ya Emerati (UAE) kwenda kuimarisha biashara ya nchi, Marekani akaenda kuzindua Sinema ya Royal Tour katika majiji ya Washington, New York na Los Angeles, mchakato uliochukua zaidi ya wiki, sasa 'ikijibu' katika biashara ya utalii kimataifa.

Baadae akawa katika ziara za uhusiano kati ya mwezi Mei na Julai huko Kampala, Uganda; Accra Ghana, Muscat, Oman; na Dakar Senegal.

Kuanzia mwezi Agosti akajumuika na wakuu wa nchi za SADC huko Kinshasa, DRC, pia akawapo katika uchaguzi mkuu wa nchini Kenya mwezi uliofuata na maziko ya Malkia Elizabeth II wa Uingereza, ikizingatiwa Tanzania ni tabaka la Jumuiya ya Madola.

Safari ya Rais Dk. Samia mwezi huo ikamfikisha Msumbiji, safari hiyo akiwa makao makuu Maputo na ziara ya 2021, alikuwa Pemba kunakoathiriwa na hali ya hewa.

Oktoba akawa Doha, Quatar kwa kikao mahsusi kuhusu afya ya umma na dunia, kisha mwezi Novemba akaendeleza uhusiano na ndugu wa taifa walioko Beijing, China na kurejea kikao cha hali ya hewa (COP) wenye hali ya hewa kama kinachoendelea hivi sasa kwa mwaka huu, hadi tarehe 22.

Kufika mwezi Desemba, Rais Dk. Samia alikuwa Marekani katika mkutano wa viongozi duniani.

### MWAKA 2023

Mapema mwaka jana. Rais alikuwa Davos Uswisi, kujadili uchumi wa dunia, kisha akarejea kikaoni kwa Waafrika wenzake huko, Dakar Senegal anakokanyaga kwa mara ya pili.

Baadaye, Februari Rais akawapo katika kikao cha Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Bujumbura, Burundi na mwezi huo akawapo Addis Ababa, Ethiopia kwa kikao cha AU.

Pia, akawa na ziara za Afrika Kusini, Windhoek, Namibia, Uganda, Nigeria kwenye uchaguzi, akakanyaga tena nchini Malawi kwenye uchaguzi, Mnamo Agosti akawa Johannesburg, Afrika Kusini, ilipofika Septemba akahudhuria kikao cha hali ya hewa mwezi huo akijadili hali ya hewa.

Pia, kukawapo kilimo cha kisasa huko Doha, Quatar na akaendeleza uhusiano ziarani India mwezi huo wa Oktoba, hali kadhalika Zambia.

Dk. Samia kaendeleza ziara hizo, akihudhuria kikao cha utalii duniani nchini Rwanda na akarejea kikao cha wakuu wa nchi wa SADC huko Luanda, Angola, kikao cha uwekezaji wa Benki ya Afrika huko Morocco na Mkutano wa Afrika, Saudi Arabia.

Kisha akarejea huko huko urabuni UAE, kuhudhuria kikao cha hali ya hewa, kilichoanza mwishoni mwa Novemba na kumalizika Desemba.

### MWAKA 2024

Taarifa za safari za rais mwezi huu zinagusa; nchi za Indonesia kudumisha uhusiano, makao makuu ya katoliki Vatican City, pia Norway; kwenye kikao cha AU huko Addis Ababa, Ethiopia; Windhoek, Namibia, Uturuki, Kenya (mkutanoni) na Ufaransa.

Pia, kuna ziara tofauti za Afrika Kusini na Rwanda, kwenye matukio ya uchaguzi; vikao vya SADC huko Zimbabwe na AU nchini Kenya katika mwezi huo wa Agosti; mwezi Septemba akahudhuria kikao cha uhusiano wa Afrika na China, kilichofanyika huko Beijng China na hivi karibuni alikuwa na kikao kingine Marekani.

TAFAKURI YA MLALAHOI




## Hebu tuache utani katika mambo makini



NA JOSEPH KULANGWA
(+255) 713 410008
kulangwasos@gmail.com

NAFIKA kijiweni nakutana na mazungumzo makali kuhusu watu kujichukulia sheria mkononi. Jamaa wanabishana, upande mmoja ukiunga mkono na mwingine ukipinga.

Wanaounga mkono wanasema wizi umekithiri na wanaokamatwa wakifika Polisi wanaachwa, ama kwa kukosa ushahidi au kwa rushwa, hivyo kurejea mitaani kusumbua watu.

Wanaopinga wanasema si ubinadamu kumpiga mtu na kumwua kwa kumchoma moto, kwa sababu wengine husingiziwa na kujikuta ama wakipoteza maisha au kupata kilema cha maisha.

Mara mmoja anaibuka na ushuhuda wa kujichukulia sheria mkononi, akihusisha na mafuta ya transfoma, akisema kuna kiongozi kadai kuwa kutokana na kukithiri wizi wa mafuta hayo, watuhumiwa wamekuwa wakinyweshwa na sasa wizi umekoma.

Sikuamini, nikamtaka arudie ushuhuda huo na kunithibitishia kuwa ni kweli kiongozi huyo kakiri kufanyika hilo, tena akionesha kufurahia hatua hiyo dhidi ya watuhumiwa wa wizi wa mafuta.

Kwa kweli bado niliendelea kutoamini kitendo hicho, huku nikifikiria pengine ni utani au maskhara ya kiongozi huyo, kama ambavyo mmoja alipata kutoa amri, kuwa shabiki wa soka asiingie uwanjani amevaa jezi ya timu pinzani ya kigeni.

Baada ya wanachi kulalamikia hatua hiyo iliyokuwa inalenga kulazimisha watu waipende na kuishangilia timu yao yaTaifa, ikimtaka kila Mtanzania anayeingia uwanjani ashabikie Taifa Stars, wananchi walitaka ufafanuzi.

Walishangaa kusikia eti atakayekwenda amevalia jezi ya timu pinzani basi lazima awe na pasipoti ikimwonesha anatoka nchi itokayo timu hiyo.

Hata hivyo hakufafanua, mpaka alipoibuka kiongozi mwingine na kudai kumbe mwenziwe alikuwa akitania!

Kwa hicho kilichokuwa utani nami nikaamini pengine hata aliyesema walinyweshwa mafuta ya transfoma alikuwa akitania, sawa na yule aliyeambia wananchi mkoani mwake, kuwa katika ziara ya Rais waibuke kwenye mikutano yake wakiwa na mabango ya kero mikononi.

Sikumbuki vizuri alikuwa nani, lakini nadhani aling'olewa uongozi wake na kurejea nyumbani.

Na kama ikitokea amerejea, nitaamini kuwa alikuwa naye anatania siku hiyo kwa wananchi wake.

Bado, wakati natafakari hayo, hili la mafuta ya transfoma liliendelea kunikereketa hasa nikihisi jinsi gani jamaa walikuwa wakifakamizwa, hasa nikikumbuka ladha ya mafuta ya taa niliyopata kuionja nikiwa mdogo.

Nikajihoji, hivi mathalan umekithiri wizi wa tindikali katika maabara zetu, je, kwa msimamo wa kiongozi wetu huyo, watuhumiwa wakipatikana watanyweshwa tindikali au itakuwaje?

Je, wezi wa nyama buchani watalishwa nyama mbichi? Wezi wa damu kwenye benki ya damu hospitalini je? Wezi wa saruji watabugizwa mifuko ya saruji ili wakome kuiba au itakuwaje?

Pengine hizo ndizo adhabu zisizozingatia utu na ubinadamu kabisa. Wakati adhabu kama hizi zikiendelea kutolewa na wenye dhamana ya

kusimamia usalama wa raia na mali zao, bila shaka tunasubiri kusikia kuwa huo ulikuwa ni utani tu na hakuna kitu kama hicho, na kama itakuwa hivyo, tutaomba kuambiwa usio utani ni upi!

Lakini kama ni kweli kuwa kuna watu walinyweshwa mafuta ya transfoma baada ya kuyaiba na si kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria ili haki iweze kutendeka, basi kuna ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu hivi sasa.

Kwa maana hiyo, bila kupepesa macho, kama hakika kuna kiongozi alishiriki kadhia hii, anapaswa kupisha na kukaa pembeni, ili sheria ifuate mkondo kwa tuhuma za mataumizi mabaya ya madaraka na ukatili dhidi ya binadamu.

Lakini endapo itashikiliwa kuwa hawakunywa bali waliigiza au kutania, basi tuamini kuwa mambo mengi yanayoahidiwa na viongozi nchini, ni utani na hayatakuja kutekelezwa kwa maslahi mapana ya nchi na watu wake.

Ndiyo kusema wananchi wenye matatizo ya msingi na waliokwisha kutoa malalamiko yao, basi wajue ahadi zinazotolewa kwao ni utani na hawatakaa wasaidiwe, bali kumwachia Mungu awaamulie mustakabali wao.

Ndugu zangu wa Kipunguni mpo? Nakusalimuni kwa jina la Kipunguni na utani uendelee!

UCHUMI

# Mkurugenzi Kafulila na darasa la Kituo Ubia inavyotekeleza PPP

**Na Joyce Lameck**

SHERIA ya Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya mwaka 2010, ilianzisha vitengo viwili ambavyo ni Kitengo cha Uratibu wa PPP kilicho chini ya Wizara yenye dhamana ya Uwekezaji na Maendeleo ya Sekta Binafsi na Kitengo cha Fedha cha PPP kilicho chini ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Mwaka 2014, serikali ilifanyia marekebisho, kwa kuunganisha vitengo viwili vilivyoanzishwa awali na kuanzisha Kituo cha Ubia maarufu kama 'One stop Center" chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mwaka 2018 Sheria ya Kituo cha Ubia, ilifanyiwa marekebisho zaidi na kubadilisha majukumu ya mpango wa kituo hicho, kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kwenda Wizara ya Fedha na Mipango.

Pia, Sera ya Ubia ilitungwa mwaka 2009 na Sheria ya Ubia ikafuata mwaka 2010, ili kutekeleza sera hiyo.

Hapo sheria nayo ikafanyiwa marekebisho kwa mara ya kwanza mwaka 2014 na mara ya pili mwaka 2018, mara ya tatu mwaka jana.



David Kafulila, Mkurugenzi wa Kituo cha Ubia. **PICHA: MTANDAO**

### MALENGO YA KITUO

Hivyo Kituo cha Ubia, kilihamishwa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu hadi Wizara ya Fedha na Mipango, ambako imeendelea kufanya kazi hadi leo, ikiwa na malengo yaliyopelekea kituo hicho kuanzishwa nchini.

Moja, ni kurahisisha uendelezaji na uratibu wa masuala yote yanayohusu utekelezaji wa programu ya PPP nchini; pia kufanya vibali kwa wakati na hivyo kupunguza muda wa usindikaji na kuondoa urudufu.

Vilevile, inatoa mwelekeo sahihi kwa mamlaka za ukandarasi na wawekezaji kupitia uundaji wa duka moja la kituo cha ubia na kuimarisha jukumu la usimamizi na usimamizi wa PPP, ili kuongeza kasi ya utekelezaji na maendeleo nchini.

Kwa sasa Kituo cha Ubia, kimeanza rasmi kufanya kazi, na David Kafulila akiwa ni Mkurungezi Mtendaji, anayeeleza namna ufanyaji kazi wao ulivyo ili kuhamasisha ubia kati ya serikali na sekta binafsi na kujenga uwezo kwa sekta binafsi.

Aidha, anataja suala la kujenga uwezo kwa mamlaka za serikali kujua namna gani wanaweza kushirikiana na sekta binafsi kwenye masuala ya ubia, hivyo kinachakata kupitia uchambuzi yakinifu zinazofanywa na pande zote mbili

### INAVYOFANYA KAZI

Kafulila anafafanua namna ubia unaweza kuwa kwenye sekta mbalimbali, ikiwamo Maji, Afya, Elimu, Barabara, Viwanja vya Ndege, Bandari na zinginezo ambazo zinaweza kuingia kwenye ubia na kuleta maendeleo makubwa katika Taifa.

Hata hivyo, Kafulila anajigamba kuwa, Sheria ya Ubia Tanzania haijawahi kupitisha mkataba mbovu, kwa sababu sheria iko makini.

Vile vile anasema uwekezaji wa sekta binafsi unahitajika, ili kuendana na ongezeko la mahitaji ya miundombinu kutokana na ongezeko la watu nchini na mahitaji ya huduma mbalimbali kuongezeka kwa wingi.

Mbinu hiyo anataja husaidia kuharakisha maendeleo na kuhakikisha huduma bora huku ikipunguza matatizo ya kifedha kwa serikali na kuhakikisha huduma zinapatikana kwa wananchi kirahisi, huku serikali ikiingiza kodi kutoka sekta husika.

Yapo manufaa ya kifedha anayotaja washirika wa kituo hicho kwa kutumia, fursa za kujenga ujuzi, jinsi namna mfumo wao thabiti wa kitaasisi na kisheria unavyosaidia utekelezaji wa PPP zilizofaulu na mada zinazofaa zaidi kama vile hadithi za mafanikio.

Anasema sekta binafsi inapoingia kwenye ubia na serikali katika kutekeleza mradi, ili kupata uwezo, uweledi namna ya kuendesha mradi husika, ndio maana tunaingia kwenye kutekeleza kwa muda tofauti kutokana na mradi husika.

Anataja inaweza kuchukua miaka mingi au kidogo kutegemea na hesabu za mradi husika zilivyo, yaani baada ya muda unaoweza kurudisha pesa na faida yake, ndipo aukabidhi mradi huo kwa serikali.

Kiongozi huyo anaeleza kuwa hadi kufikia sasa takribani miradi 74, ambayo ipo kwenye hatua mbalimbali za utambuzi kwenye sekta tofauti, mfano mradi wa barabara ya mwendo kasi Kibaha, Chalinze ambao kwa sasa upo kwenye hatua ya tathimini.

Aidha, anaeleza sifa kubwa ya sheria ya ubia Tanzania, ni yenye uwazi na yenye ubora inayoweza kuhakikisha maslahi ya umma na kampuni binafsi yanapatikana, yaani inaleta faida pande zote mbili.

Kafulila anasema, kuna umuhimu wa kubadilisha mtazamo wa umma kutumia ubia kufanya mradi wa serikali, ili kuepusha gharama kwa serikali ambazo zinaweza kufanywa na sekta binafsi, ili kudumisha miundombinu na huduma za umma zinazohitajika.

## Wizi madini waumiza kichwa Shinyanga, imejipanga kwa makali ya kisu

**INATOKA UK.11**

Mwenyekiti Mpya Soko la Madini, Mkoa wa Kimadini Kahama, Zabroni Ngereja, akichukua nafasi ya aliyekuwapo, anasema wamefanikiwa kudhibiti tatizo la utoroshaji madini uliokuwapo hapo awali kwa asilimia 99.

Anatahadharisha kwamba, mfanyabiashara atakayebainika kujihusisha na vitendo hivyo vya utoroshaji madini, iwe ndani ya soko, maeneo ya wachimbaji au kufadhili utoroshaji, watamuondoa asiendelee kufanya biashara hiyo na kutowachafua.

"Utoroshaji wa madini ambao upo kwa sasa hivi ni kwenye maeneo ya machimbo madogo, ukiwamo mgodi wa Nyangarata, Nyikoboko,Nyamishiga, Masabi na maeneo mengine. Huko ndipo serikali inapaswa kwa sasa kuwekeza nguvu nyingi,"anasema Ngereja.

### MCHIMBAJI

Mchimbaji Mdogo wa madini kutoka machimbo ya Mwime Kahama, Joseph Masunga, anasema tatizo la utoroshaji madini linasababishwa na uchache wa masoko na tozo nyingi.

Mfanyabiashara wa madini Mpanzu Nswila, anasema kwamba utoroshaji huo wa madini ni hasara kwa taifa kwa kukosa mapato na kushindwa nchi kunufaika na rasilimali zake na kunufaisha mataifa mengine.

RPC SHINYANGA

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga Janeth Magomi, anasema wamekuwa wakikamata watu wanaojihusisha na utoroshaji wa madini, na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.

Anasema walishakamata watu sita wakitorosha madini ya dhahabu wilayani Kahama, yenye uzito wa gramu 930.88 yenye thamani ya Sh. milioni 93.

Anasema uchunguzi wa awali, walibaini watuhumiwa hao walikuwa wakitorosha madini kuyapeleka nje ya nchi, kwa lengo la kukwepa kulipa kodi na tozo za Serikali, kitendo ambacho ni kosa kisheria.

"Tatizo hili la utoroshaji madini lipo sana katika wilaya ya Kahama. na sisi kama Jeshi la polisi tumekuwa tukifanya msako na doria mbalimbali na kuwakamata watuhumiwa wakitorosha madini na kuwafikisha mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria,"anasema Magomi.

### MKUU WA MKOA

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Anamringi Macha, anasema tamko la waziri wa madini Anthony Mavunde, kusema mkoa wa kimadini Kahama unaongoza kwa utoroshaji wa madini ni aibu kwa mkoa, na kwamba na siyo habari njema bali wanapaswa kudhibiti tatizo hilo.

Anasema tayari wameshabaini maeneo mbalimbali ambayo hufanyika biashara hiyo haramu ya utoroshaji madini, ikiwamo kwenye viwanda vya kukoboa mpunga.

"Biashara ya utoroshaji madini ambayo inafanyika Kahama hufanyika pia kwenye viwanda vya kukobolea mpunga, wakati shughuli za kukoboa zikiendelea kumbe kuna madalali wanafanya biashara haramu za madini, hii ni aibu kwetu kama mkoa," anasema Macha.

Anasema katika misako ambayo wanaendelea nayo ya kudhibiti mianya ya utoroshaji madini, kwamba wakikuta biashara hiyo haramu ikiendelea tena kwenye viwanda vya kukoboa mpunga, wahusikawatachukuliwa hatua kali za kisheria kwa kuruhusu biashara hizo.

Anasema, mkoa wa kimadini Kahama unafanya vizuri katika uzalishaji wa madini, lakini tatizo jingine ni soko la madini kuzidiwa, na kuagiza iwekwe mikakati ya kuongeza ukubwa wa soko hilo, ili kudhibiti tatizo la utoroshaji wa madini na watu kuuza mali katika masoko hayo.



# Maofisa ardhi wa mikoa kikaangoni

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi amewaagiza makamishna wa ardhi wa mikoa nchini kuwasilisha ofisini kwake taarifa kila mwezi walivyotatua migogoro ya ardhi kwenye maeneo yao.

Akizungumza jana kwenye kikao kazi cha makamishna hao na wenyeviti wa mabaraza ya ardhi nchini, Ndejembi, alisema wanapaswa kuhakikisha hati zinatolewa kwa wakati na hakuna migogoro mipya ya ardhi inayozalishwa kwenye maeneo yao.

"Natamani wote tuwe na uwezo wa kuyaona na kutatua mambo kabla hayajawa au kutuletea shida, kwa hiyo kila mwezi mtuletee ripoti kupitia kwa Katibu Mkuu ili tuweze kujua nini kinaendelea," alisema Ndejembi.

Alielezea jinsi wananchi walivyokosa imani na baadhi ya mabaraza ya ardhi nchini kutokana na utendaji wao na kutoa maamuzi yanayoegemea upande wenye fedha. "Kwasasa tukifanya dodoso kwa wananchi huko nje kuhusu mabaraza wengi watakwambia hatuna imani, kwanini hawana imani kwa kuwa mara nyingi mwenye nacho ndio hutoka na haki," alisema Waziri huyo.

Kwa upande mwingine, alionya tabia ya watumishi wa ardhi wanaovujisha siri na kusema uchunguzi unaendelea dhidi yao na watakaobainika watawajibishwa.

Msajili Msaidizi wa Mabaraza ya Ardhi, Dorothy Moses, alisema wamejipanga kuhudumia ipasavyo mwananchi anayefika kutafuta haki kwenye mabaraza ya nyumba ya wilaya na mikoa.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi mkoani Mwanza, Happiness Mtutwa, alisema baada ya kikao hicho watakaa na watumishi walio chini yao kuwapa maelekezo ili utendaji wao uwe na tija.

**"Ulaya reli ni ya serikali, mabehewa ni ubia, hivyo tuipe nafasi sekta binafsi ishiriki katika reli ibebe mizigo. Pia nashauri vipande vilivyobaki vya kujenga serikali isibebe...**



Polisi wa Usalama Barabarani akiamuandikia cheti cha kulipa faini dereva wa gari la kubeba mizigo katika eneo la Kamata jijini Dar es Salaam baada ya kudaiwa kukiuka sheria za barabarani **PICHA:JUMANNE JUMA**

# Wananchi waachwe wachague viongozi wanaowataka- Askofu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Pentecostal Holiness Association Mission Tanzania (PHAMT), Nkumbu Mwalyego amezitaka mamlaka kuwaacha wananchi kuamua kuchagua viongozi bora katika uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika nchini Novemba 27, mwaka huu.

Mwalyengo alitoa rai hiyo juzi jijini hapa kwenye ibada maalum ya uzinduzi wa gari na kutumia fursa hiyo kuhimiza wananchi waliojiandikisha kwenye daftari la mkaazi nchini kujitokeza kupiga kura kwenye uchaguzi huo wa wenyeviti wa mitaa, vitongoji, vijiji na wajumbe wao. Alisema jukumu la kuwapata viongozi ni la wananchi na siyo mamlaka kuwapangia mtu wa kumchagua ama kutomchagua.

"Taifa linahitaji kuwapata viongozi waaminifu na kuitumikia nchi yao katika misingi ya uwajibikaji na utawala bora na kukemea vitendo viovu vikiwemo vya rushwa na vya ukatili wa kijinsia," alisema.

Alisisitiza suala la kuwapata viongozi bora liachiwe kwa wananchi ambao wamejiandikisha kushiriki katika uchaguzi huo utakaovishirikisha vyama vya siasa nchini.

"Uchaguzi wowote unaofanyika unahitaji kupata mabadiliko ya kuwapata viongozi walio sahihi na siyo watakaokuwa vikwazo kwa wananchi, hivyo kuna ulazima wa kuwapatia fursa wananchi kuwachagua wanaoona wapo sahihi kuwaongoza," alisema.

Vilevile, Askofu huyo aliwataka Watanzania kutumia vipato vyao kuwekeza kwenye miradi ili kujikwamua kiuchumi na kuondokana na umaskini ambao umekuwa kikwazo kubadili mfumo huo wa maisha yao.

Awali, Mchungaji Kiongozi wa kanisa hilo, James Mwampona, alisema katika kuunga mkono juhudi za serikali, wameibua miradi ikiwamo kilimo cha zao la korosho na ununuzi wa eneo kwa ajili ya ujenzi wa shule.

Mwampona, alisema, kanisa hilo limedhamiria kuhakikisha linawafikia wananchi kiroho na kiuchumi na kuahidi kushirikiana na serikali kuwaletea maendeleo.

Kuhusu gari, alisema litatumika kuwafikishia neno la Mungu waumini wa kanisa hilo na kufanya shughuli mbalimbali za kijamii na kujipatia kipato.

"Sisi kama washarika wa Kanisa hili tunaamini kuwa ununuzi wa gari hili lenye thamani ya Sh. milioni 45 litatuwezesha kuifanya kazi ya Mungu kwa ufanisi na hii itaweza pia kuisaidia jamii na serikali katika kuleta maendeleo,"alisema

# Taasisi yalilia mikopo ya asilimia 10 kwa wenye ulemavu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kuwajengea uwezo watu wenye ulemavu kutumia mifumo itakayotumika kutoa mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri nchini ili wanufaike ipasavyo na fursa hiyo.

Mkurugenzi wa Taasisi inayojihusisha na masuala ya watu wenye ulemavu nchini ya Foundation for Disabilities Hope (FDH), Michael Salali alitoa ombi hilo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Salali, alisema kundi kubwa la watu wenye ulemavu nchini bado wapo nyuma katika matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

"Mapindizi makubwa ya matumizi ya mitandao ambayo ina faida na changamoto zake kundi la wenye ulemavu bado lipo nyuma kwenye matumizi ya kiteknolojia na mitandao kutokana na sababu mbalimbali za kiulemavu walizonazo.

"Mfano mweye ulemavu wa kutosikia (kiziwi) yeye hawezi kuendana na teknolojia inamuacha pembeni kwa sababu taarifa zinachelewa kumfikia kwa kuwa yeye anatumia lugha ya alama au ndugu zetu wasioona (vipofu) wanapotaka kuingia kwenye hiyo mifumo wanakutana na vikwazo kutokana na changamoto zao za kiulemavu" alisema Salali.

Akizungumzia kuhusu mikopo hiyo, alisema walikuwa wakisubiri kwa muda mrefu, lakini limekuja na kikwazo chanagamoto ambazo kama hazifanyiwa kazi wenye ulemavu hawata nufaika.

"Kuna mfumo umetengenezwa ambao tunaweza kuomba mikopo mtandaoni kweli hapo kuna changamoto, tunataka tuwajengee uwezo ili tuone namna ya kuweza kutumia ule mfumo waweze kukopa," alisema.

Akizungumzia wasioona, Salali, alionya halmashauri na serikali zisipowekea mkakati maalumu, halitanufaika na mikopo hiyo kwani ni ngumu kwao kutumia mifumo ya mitandao.

Alisema taasisi hiyo inatarajia kukutana na viongozi wa halmashauri nchini ili kuwasaidia wenye ulemavu wanufaike na mikopo hiyo.





# Wafugaji wahaha kupata malisho

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

VIONGOZI wa mila wilayani hapa Mkoa wa Mbeya wameiomba serikali iwagawie wafugaji vitalu kwenye Shamba la Mifugo (NARCO) la Usangu ili kudhibiti baadhi yao kuvamia Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kuibuka mgogoro baina yao.

Viongozi hao wa kabila la Wamasai (Maleigwanani), Wasangu (machifu) na wasukuma (watemi) walisema wafugaji wanapeleka mifugo hifadhini kwa lengo la kutafuta maji na malisho.

Walitoa ombi hilo wakati wa kikao kazi na maofisa wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kujadili kudhiti uingizaji mifugo kwenye Bonde la Ihefu lilipo ndani ya hifadhi hiyo ya Ruaha.

Mmoja wa viongozi hao, Makresia Pawa ambaye ni Mwenyekiti mstaafu wa Chama cha Wafugaji Wilaya ya Mbarali, alisema migogoro kati ya wafugaji na hifadhi ilianza muda mrefu na kusababisha mauaji.

Pawa, alisema eneo pekee ambalo wafugaji walitakiwa wafuge mifugo yao ni kwenye shamba hilo ambako hakuna hata mmoja wa wilaya hiyo amemilikishwa kitalu zaidi ya wageni kutoka maeneo mengine.

Alisema wengi waliomilikishwa vitalu hivyo sio wafugaji na kugeuza kwa ajili ya kilimo cha mpunga.

"Hata kwenye vijiji hakuna yaliyotengwa wafugaji, maeneo machache yaliyokuwa yametengwa yanabadilishwa matumizi na viongozi wa vijiji na kusababisha wafugaji kutokuwa na maeneo," alisema Pawa.

Katibu wa Chama cha Wafugaji Wilaya ya Mbarali, Barick Julius, alisema eneo kwa ajili ya mifugo katika wilaya hiyo linatosheleza mifugo 60,000.

Julius, alisema mifugo iliyopo ni zaidi 220,000, hivyo wafugaji kukosa maeneo ya kufugia.

**"Hata kwenye vijiji hakuna yaliyotengwa wafugaji, maeneo machache yaliyokuwa yametengwa yanabadilishwa matumizi na viongozi wa vijiji na kusababisha wafugaji**

Alisema chama hicho kimekuwa kikifanya kazi kwa kushirikiana na serikali kuhakikisha wafugaji wanapata huduma muhimu.

Alisema wamekuwa wakiandika maandiko mara kwa mara wakiomba serikali iwapatie eneo la NARCO ili walitumie, lakini haijawahi kuwajibu.

"Tunaomba tusaidiwe lile eneo kwani ni pekee linaweza likatusaidia kupunguza migogoro, eneo la hifadhi ni muhimu sana kwahiyo hata sisi hatutaki mifugo iingie huko," alisema .

Mkuu wa Hifadhi ya hiyo ya Ruaha, Godwell Ole Meing'ataki aliwapiga marufuku wafugaji kuendelea kuingiza mifugo ndani ya bonde hilo la Ihefu, lasivyo watachukuliwa hata kali.

Meing'ataki, alisema wanaendelea kufanya oparesheni ndani ya hifadhi hiyo kwa lengo la kuzuia uharibifu wa mazingira unaofanywa na wafugaji hao ili kulinda ikolojia ya hifadhi na Mto Ruaha Mkuu.

"Tumeamua kuanza kufanya vikao na nyie viongozi wa wafugaji kwa sababu ninyi mnaaminiwa nao, nendeni mkawaambie wasipeleke mifugo hifadhini kwa sababu tutaendelea kuchukua hatua," alisema Meing'ataki.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbarali, Frank Sichalwe, aliwataka wafugaji wa wilaya hiyo kupunguza idadi ya mifugo ili kudhibiti migogoro ya mara kwa mara kutokana na uhaba wa maeneo ya malisho.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera Bunge na Uratibu) William Lukuvi ambaye ni mbunge wa Isimani mkoani Iringa akizungumza na wananchi katika mikutano tofauti katika ziara yake kata ya Kising'a Tarafa ya Isimani jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijiji vyaula, vyapimiwa ardhi Busokelo

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

TUME ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imeanza kupima upya mipaka ya vijiji 14 vya kata nne za Halmashauri ya Busokelo Wilaya ya Rungwe mkoaniMbeya kwa lengo la kutatua migogoro ya ardhi baina ya wananchi na Hifadhi ya Taifa ya Kitulo.

Meneja wa Tume hiyo Kanda ya Kusini, Pili Msati alisema kazi hiyo inafanyika kupitia Mradi wa Uboreshaji na Usalama wa Miliki kwa lengo la kuwasaidia wananchi kuwa na matumizi bora ya ardhi.

Pili, alisemawananchi watakaonufaika na mradi huo wilayani humo watasaidiwa kupanga matumizi ya ardhi yao na kuainisha mipaka ya maeneo yao ili kumaliza migogoro ya ardhi baina yao.

"Tunapima ardhi ya wananchi kupitia mradi huu wa Uboreshaji na Usalama wa Miliki, lengo kubwa ni kuwasaidia kupanga matumizi ya ardhi yao, tukimaliza kupima tunaamini migogoro ya ardhi baina ya wananchi na hifadhi na hata ile miongoni mwao itakuwa imekwisha," alisema Pili.

Maofisa watendaji wa vijiji vya Mwela na Kilasi vilivyopo kata za Kandete na Luteba, walisema zoezi hilo litakuwa na manufaa makubwa kwa wananchi kwa kuanza kutumia ardhi kiuchumi.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mwela, Pendo Mwasajile, alisema mradi huo ukikamilika utawasaidia wananchi kujua maeneo yaliyotengwa kwa kilimo, ufugaji na biashara na kuondoa migogoro miongoni mwao.

# Mbeya-WSSA yatangaza bingo watakaofichua wezi wa mita

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU wasiojulikana wameanza kuiba dira za maji na kuharibu miundombinu kwenye makazi ya maeneo ya Jiji la Mbeya na kusababisha wananchi kukosa huduma.

Kutokana na hali hiyo, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), imetangaza kutoa zawadi ya Sh. 1,000,000 kwa mwananchi atakayetoa taarifa na kuwatia mbaroni wahalifu hao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mbeya-WSSA, Gilbert Kayange alitangaza bingo hiyo juzi wakati wa ziara ya kukagua miundombinu ya maji kwenye baadhi ya maeneo ya jiji hilo na kusikiliza kero za wananchi kuhusiana na huduma hiyo.

Katika ziara yake, Kayange alitembelea maeneo ya Sae, Iyunga, Forest, Isyesye Novwe na Iyela ambayo ni miongoni mwa maeneo ambayo yamekuwa yakikumbwa na tatizo hilo mara kwa mara.

Alisema baadhi ya wahalifu hao walikamatwa na mamlaka hiyo kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama na kufikishwa mahakamani kwa makosa hayo.

Alisema mamlaka hiyo mbali itatunza siri kwa mwananchi atakayetunza siri ili kuepuka uhasama miongoni mwa wanajamii.

"Hili tatizo tunalijua na tulishaanza kuchukua hatua, wapo ambao tulishawafikisha mahakamani na tukawafungulia kesi za uhujumu uchumi kwa sababu hili vitendo hivi vinasababisha hasara kubwa," alisema Kayange.

Alisema baadhi ya maeneo wananchi wasiokuwa waaminifu wamekuwa wakiiba maji kwa kujiunganishia kwa kuchepusha yasipite kwenye dira.

Awali baadhi ya wananchi, walisema wahalifu hao wamekuwa wakiiba dira hizo usiku wakati wamelala na kuwawia vigumu kuwabaini na kuwakosesha maji.

Mmoja wa wananchi hao, Sophia Mwamburuma,Mkazi wa Sae, alisema haijulikana, wahalifu hao wanakwenda kufanyia kazi gani dira hizo wanazoiba.

Sophia, alisema wengi wamelazimika kuhamisha dira kutoka nje na kuziweka ndani ya uzio ili kuepuka kuzibiwa na kukosa maji.

"Kuna wakati walikuwa wanaiba mabomba lakini kwa sasa tatizo kubwa liko kwenye dira, wanakuja usiku wanazifungua na kuondoka nazo, unakuta asubuhi maji yanamwagika," alisema Sophia.

Safari Mbilinyi, aliwaomba viongozi wa Mbeya-WSSA kufuatilia ili kubaini dira hizo zinatumika kwenye shughuli na kudhibiti wezi.

Alisema awali wezi wa mabomba walikuwa wanauza kama chuma chakavu na huwa ni rahisi kufuatilia tofauti na dira.

Wizi wa dira na uharibifu wa miundombinu mingine ya maji ni miongoni mwa visababishi vya upotevu wa maji na hasara Mbeya-WSSA.



# Walaani picha za video kukiuka maadili mitandaoni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMATI ya Wataalamu wa Habari Zanzibar (ZAMECO) imelaani picha ya video kusambaa kwenye mitandao ya kijamii baada ya kufanyika Zanzibar ikionesha wasichana wawili wanaulizwa maswali yanayokiuka maadili, kuvunja heshima na haki za binadamu.

Kamati hiyo inaundwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA- Zanzibar), Baraza la HabariTanzania (MCT), Jumuiya ya Waandishi wa Habari za Maendeleo Zanzibar (WAHAMAZA), Jukwaa la Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC Zanzibar) , Klabu ya Waandishi wa Habari Zanzibar (ZPC) na Klabu ya Waandishi wa Habari Pemba (PPC).

Kwa mujibu wa taarifa hiyo iliyosainiwa na Dk. Mzuri Issa, Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, tukio hilo limeibua hisia kali kwa wadau wa habari, watetezi wa haki za binadamu na jamii na kuibua maswali yasiyo na majibu miongoni mwa wanahabari kuhusu maadili, haki za binadamu, na misingi ya uhuru wa vyombo vya habari.

Katika taarifa hiyo, ZAMECO inasisitiza kuwa vitendo vya udhalilishaji kwa watoto wa kike na jamii ni ukiukwaji wa haki za binadamu, maadili ya uandishi wa habari na kuvuruga mipaka ya uhuru wa kujieleza ambao unalindwa na kuhitajika kutoa habari sahihi na kuibua mijadala yenye tija na manufaa kwa jamii.

**Alisema hiyo ina maana kuwa uhuru wa vyombo vya habari unaendana na jukumu la kuheshimu utu wa kila mtu, hususani wanawake na vijana ambao ni waathirika wa moja kwa moja katika ...**

"Kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR 1996) Ibara (19) kila mtu ana uhuru wa kutoa taarifa bila ya kuathiri haki ya mtu na amani ya nchi," alisema Dk. Mzuri.

Alisema hiyo ina maana kuwa uhuru wa vyombo vya habari unaendana na jukumu la kuheshimu utu wa kila mtu, hususani wanawake na vijana ambao ni waathirika wa moja kwa moja katika hatari itakayotokea.

Alisema ZAMECO inaitaka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Tume ya Utangazaji Zanzibar kuhakikisha maudhui yanayorushwa na vyombo vya habari na mitandao hiyo yanaendana na maadili, uwajibikaji na kulinda jamii dhidi ya maudhui yenye madhara kwao, kama vile yaliyomo yanayokiuka haki za binadamu, kudhalilisha au kuchochea vurugu na chuki.

Hata hivyo, alisema ZAMECO inaitaka Wizara ya Habari, Utamaduni, Vijana na Michezo Zanzibar kuharakisha upatikanaji wa sheria mpya ya huduma za habari nchini kwa lengo la kupunguza changamoto kama hizo ambayo ni kilio cha muda mrefu kwa waandishi, wahariri na jamii.

Kwa upande mwingine, alisisitiza kuwa kamati hiyo inasisitiza umuhimu wa wasichana kujitambua, kujithamini na kujiwekea malengo ambayo yatasaidia kuboresha maisha yao na jamii

Alisema ZAMECO pia inawataka wazazi na walezi kuwa mstari wa mbele kuwaelimisha watoto wao wa kike juu ya thamani yao, haki zao na nafasi yao katika jamii.



Rais wa Zanzibar Dk Hussein Ali Mwinyi akimuapisha Iddi Said Khamis kuwa Kadhi wa Mahakama ya Kadhi ya Rufaa Zanzibar, hafla hiyo ilifanyika katika ukumbi wa Ikulu jijini Zanzibar jana. Kushoto kwa Rais ni Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Mhandisi Zena Ahmed Said. **PICHA: IKULU**

# Unguja, Pemba waongoza ulaji samaki

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Shaabani Ali Othman amesema wananchi visiwani hapa wanaongoza kwa ulaji wa samaki kwa kila mmoja kwa kilo 22 kwa mwaka.

Othman, alisema kuwa kiwango hicho ni kikubwa ikilinganishwa na ulaji wa samaki duniani ambao kwa mtu mmoja ni kilo 21 kwa mwaka.

Akizungumza katika Mkutano wa Mtandao wa Afrika wa usalama wa samaki na matumizi ya teknolojia ya uvuvi uliozishirikisha nchi 20 za bara hilo, alisema wananchi hao wamefikia vigezo vya dunia kwa ulaji samaki kutokana na kuvuliwa wengi visiwani hapa.

Othman, alisema uvuaji samaki Zanzibar umefikia tani 100,000 kwa mwaka huu kutoka 80 za mwaka jana.

Alisema idadi hiyo ni kubwa kutokana na kuongezeka kwa ulaji wa kitoweo hicho kwa wananchi wake.

Alisema ulaji huo utasaidia upatikanaji wa protini kwa wananchi na kujenga afya nzuri kwa kuwa samaki hutumika kama sehemu ya chakula katika milo yao.

"Mkutano huu ni jambo la faraja kufanyika hapa visiwani Zanzibar kwa vile visiwa hivi vimezungukwa na bahari na kuna wavuvi wengi,"alisema.

Othman, alisema mkutano huo pia utajadili namna ya Zanzibar itakavyopambana na uvuvi haramu dhidi ya wavuvi katika maeneo tofauti.

Alisema wananchi wengi wamekuwa na mwamko wa kutumia zana za kisasa za uvuvi kwa kuvua samaki waliokomaa kisheria. "Tunaposema usalama wa chakula cha samaki ni samaki wanaoongeza protini ya afya ya binadamu ambao ndio wanaohitaji kuvuliwa," alisema Waziri huyo. Mkurugenzi Mkuu wa Tasisi ya Utafiti wa Mazao ya Baharini, Dk. Zakaria Ali Khamis, alisema Zanzibar inalinda usalama wa samaki kwa kutoa elimu kwa wavuvi kuachana na uvuvi haramu na kuvua samaki waliokomaa.

Mtaalamu wa Uvuvi, Hashim Chande Muumin, alisema serikali imetoa miongozo ya uvuvi kwa kuwataka wavuvi kuvua samaki waliokomaa kisheria ili kuepuka wachanga.

Muumini, alisema kufanyika kwa mkutano huo visiwani hapa kutainufaisha Tanzania kwa kupata tafiti ambazo zitasaidia kukabiliana na matatizo yaliyopo duniani na Zanzibar.

Alisema kwa upande wa wananchi, watapata teknolojia rafiki kupunguza upotevu wa samaki kwa wavuvi.

## Ajali barabarani janga Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Ujenzi, Mawasilinano na Uchukuzi imesema Serikali ya Zanzibar inaimarisha mtandao wa barabara visiwani hapa ili kuondokana na janga la ajali za barabari na kunusuru maisha ya wananchi na majeruhi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Khalid Salum Mohamed

wakati akizungumzia Madhimisho ya Wiki ya Usalama Barabarani visiwani hapa ambayo kwa mara ya kwanza yanaanza kufanyika Novemba 16 (kesho) hadi Novemba 23, mwaka huu.

Mohamed, alisema wakati wa maadhimisho, watatoa elimu ya usalama wa barabarani kwa wananchi ili kudhibiti ajali zisizokuwa za lazima.

Alisema ajali za barabarani, limekuwa janga kubwa visiwani hapa na linahitaji uelewa wa pamoja kwa watu wote ili kutokomeza na kufikia malengo ya serikali iliyojiwekea katika Dira ya Maendeleo ya 2050.

Huku akinukuu Mkataba wa Usalama Barabarani Afrika Mohamed, alisema unazitaka nchi wanachama kuunda mabaraza ya usalama kuratibu shughuli za usalama barabarani katika nchi zao kwa kuzingatia sheria namba 10 ya mwaka 2019 ya usafiri barabarani na marekebisho yake.

Waziri huyo aliwataka watendaji wa wizara yake kuunda kamati ya kitaifa ya usalama barabarani yenye wajumbe kutoka sekta za usafiri wa barabarani visiwani hapa.

Alisema kuwa maadhimisho hayo ya kwanza kufanyika visiwani hapa yatapata ufanisi na kufikia lengo la kuanzishwa kwake.

"Tumejipanga kuhakikisha kuwa tunafanya vizuri wiki hiyo, licha ya kuwa Zanzibar ni kwa mara ya kwanza, " alisema Dk. Khalid.

Alisema wizara hiyo kupitia Kamati ya Kitaifa ya Usalama Barabarani imepanga kuadhimisha wiki hiyo yenye kaulimbiu ya maadhimisho hayo kuwa ni "Utekelezaji wa Mkakati wa Usalama Barabarani Zanzibar 2024-2030 ni suluhisho la ajali za barabarani"

Alisema lengo kuu la maadhimisho hayo ni kuendelea kutoa elimu ya matumizi sahihi ya barabara na kuwaelimisha wananchi juu ya janga la ajali za barabarani linaloendelea kuikumba Zanzibar.

"Katika kipindi chote cha maadhimisho hayo shughuli mbalimbali zitafanyika ikiwemo kongamano ,usafi wa mazingira, kutoa elimu juu ya matumizi sahihi ya barabara na uchangiaji wa damu kwa hiyari," alisema Waziri huyo.

Alisema pia kutakuwa na maonesho katika viwanja vya Kisonge Mnarani kwa kushirikisha taasisi za Serikali na binafsi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOSEPHINE WILLIAM NIKOMBOLWE** anatangaza kupotelewa na cheti cha darasa la saba chenye index namba **407015-084** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **TUMBI PRIMARY SCHOOL** mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/PWA/KIB/24534/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**LEONARD DAVID MAGOMBA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 342 DKG - DYNA. KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 512 DDX - MITSUBISHI CANTER. KWA YEYOTE ATAKAEZIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DAR/KIN/250327/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CHRISTIAN LEONARD MAKOMBE,** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 221 DZW AINA YA SUZUKI ESCUDO, CHASSIS NO. TDA4W201795, ENGINE NO J24B10576889. YEYOTA ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DAR/UBU/175897/2024.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Kawe Wilaya ya Kinondoni**
**Shauri la Madai Na....586...2024**
**Jina la Mdai Mwalimu Kashasha Foundation (Godwills)**
**Jina la Mdaiwa Smile Sasa (T) Limited (Jeremiah Mayenga)**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za Taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: Smile Sasa (T) Limited (Jeremiah Mayenga) wa Mikocheni**
Kwa kuwa Mdai/Wadaiwa ameleta/wameleta madai yake/yako kwamba (Eleza hapa habari za madai) **YA PESA TSH. 7,500,000/= FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA KATIKA TAREHE ULIO PANGIWA** kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 25 mwezi 11 Mwaka 2024 saa 2:30 Asubuhi Mbele ya Mh. Massengi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hii ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vinavyohusika shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**Angalizo:** Kama hautahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini. Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri ya Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 13 Mwezi 11 Mwaka 2024
Sahihi ya Mdaiwa........................

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No 26172 Of 2024**
**In the Matter of the estate of the late**
**PETRO JAMES KATEKETA of Kikuyu within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by TITUS PETRO KATEKETA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 19 day of 11......2024
Dated at Dodoma this 31 day of 10..........2024

.... RESIDENT MAGISTRATE ......

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASIJALA MDOGO SHINYANGA**
**ILIYOPO SHINYANGA**
**MAOMBI YA ARDHI NA.25886 YA 2024.**

**WILLIAM SWAI.**

**DHIDI YA**

**1.REGINA ROBERT KISHIGA.**
**2.SILAS M. LAZIMA.**

**KWA; SILAS M. LAZIMA.**
**POPOTE ULIPO.**
Unajulishwa kwamba rufaa tajwa imepangwa kutajwa mnamo tarehe 03.12.2024 saa 3:00 asubuhi, mbele ya Mhe.N.L. Mwakahesya, J.
Hivyo unaamriwa kuhudhuria siku hiyo bila kukosa na kama hutahudhuria maombi haya ya ardhi yatasikilizwa na kutolewa uamuzi bila wewe kuwepo.
Imetolewa kwa amri yangu na kupigwa chapa ya Mahakama leo tarehe 11.11.2024.

.........................
**A.H. MWETINDWA**
**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA SHINYANGA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi Na 1764 .... /20.............2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU MOHAMED KHAMIS MOHAMED WA.........**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA MASHAKA ISSA MSALANGI**


**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 19 Mwezi 11 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

Imetolewa leo Tarehe 04 Mwezi 11 Mwaka 2024

## KUPOTEA KWA HATI YAKUSAFIRIA



**JESCA DAVID KISHOA,** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA HATI YAKUSAFIRIA YENYE NAMBA **TDE012459** ILIYOTOLEWA NA IDARA YA UHAMIAJI PCO DAR ES SALAAM **TAREHE 17/06/2021,** YEYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/52189/2024**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.26147 OF 2024**
**IN the Matter of the late:**
**GEORGE LEVI MWAMENGELE**

**1. NAOMI WILLIAM MWAIKAMBO**
**2..............................................**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above-named pepetitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 18 day of 11,2024.
Dated at Morogoro this 04 day of 11, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

***OFISI ZA MATANGAZO***
***Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.***
***Mobile: +255 - 745 700 710.***
***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***
***Website: www.ippmedia.com***

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

## MIRADI KUSUASUA... Waingiwa hofu wananchi kususa kupiga kura

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

MADIWANI wa Halmashauri ya Chalinze, wilayani Bagamoyo wamezikumbusha taasisi za umma kutekeleza wajibu wake kwa kutatua vikwazo vilivyopo kwa wananchi kwa wakati, zikiwamo upatikanaji huduma za maji na barabara.

Wamesema kukosekana kwa huduma muhimu kwa wananchi ni moja ya sababu zinazowafanya baadhi yao kutokuwa na ari ya kwenda kupiga kura.

Madiwani walieleza hayo juzi wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani cha robo ya kwanza ambacho pamoja na mambo mengi, walijadili kukosekana huduma za kijamii karibu na wananchi, jambo ambalo linawapa hofu ya kutopata kura nyingi kwa wagombea wakati wa Uchaguzi Serikali za Mitaa.

Diwani wa Talawanda, Ramadhani Bigga alieleza katika kikao hicho kuhusu kukosekana maji kwenye baadhi ya maeneo katika kata yake huku mabomba yakiwa yamelazwa chini kwa muda mrefu.

Diwani wa Vigwaza, Mussa Gama alihoji kuhusu ukosefu wa maji kwa mwezi mmoja sasa katika maeneo ya kata hiyo huku kukiwa hakuna taarifa za jitihada zinazofanywa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salam (DAWASA).

Gama alisema kukosekana maji kwa muda mrefu kumeleta malalamiko kwa wananchi wa eneo hilo katika vijini vya Vigwaza, jambo ambalo aliomba DAWASA kutoa ufafanuzi wa utatuzi wake.

Meneja wa DAWASA Chalinze, Abraham Mwanyamaki alieleza katika kikao hicho kwamba, kukosekana maji kwa baadhi ya maeneo kumechangiwa na tatizo la umeme ambalo hivi sasa linafanyiwa kazi kurejesha huduma ya maji kwenye maeneo hayo.

Akizungumzia miundombinu iliyosambazwa na mingine ambayo imeunganishwa na maji hayatoki katika maeneo mbalimbali, ikiwamo kata ya Talawanda na Mbwewe Mwanyamaki, alisema kazi ya kuunganisha maji itafanyika na kwamba mipango inaendelea kufanywa na ofisi hiyo.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Ramadhani Possi alisema ametenga Sh. milioni 800 kwa ajili ya ufungaji taa za barabarani katika vituo sita vya halmashauri hiyo, vikiwamo Ruvu Darajani, Ubena, Mdaula, Kibindu na Miono.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Hassan Mwinyikondo alisema ulipaji fidia kwa kata saba za eneo lilikojengwa soko la Bwilingu, umeanza na tayari kaya mbili zimeshakamikishiwa malipo.

# Askofu awaonya waumini wanaokimbilia miujiza

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BAADHI ya viongozi wa dini barani Afrika wameitaka serikali kuungana na madhehebu ya dini kuunda chombo maalumu kwa ajili ya kudhibiti manabii na wachungaji wanaotoa mafundisho ya uongo ambayo yamekuwa yakipotosha waumini nchini na Afrika kwa kuwaingiza katika matatizo, vikiwamo vifo.

Walitoa kauli hiyo jana jana jijini Mwanza wakati wa mjadala wa Kiekumene kuhusu imani moja na mafundisho sahihi kwa ustawi wa maisha ya mwanadamu ulioandaliwa na Chuo cha Biblia Kilutheri Nyakato kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT).

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini Magharibi, Dk. Abednego Keshomshahara alikemea waumini wanaotegemea zaidi miujiza, akionya kuwa wanasahau kuwa Mungu aliyetaka waombe ndiye huyo aliyetaka wafanye kazi.

"Wapo waumini wanaoona kuwa kuombewa kwa kila mtumishi ndiyo maisha, utaona kila ninaposikia mahubiri yeye yupo anatumia zaidi fedha katika kutafuta kuombewa, anasahau kuwa Mungu mwenyewe amesema aombaye hupewa na si aombewaye hupewa. Achene kushikilia mahubiri ya uongo," alionya Askofu Keshomshara.

Alionya kuwa kutegemea zaidi miujiza ni upotoshaji, hivyo kuwata waumini kutumia muda wao kufanya shughuli za kiuchumi na kuacha kutumia muda mrefu katika kutegemea mazingaombwe na miujiza ya upotoshaji.

Mhadhiri wa Falsafa wa SAUT, Padre Dk. Innocent Sanga, alisema kuwa hivi sasa mafundisho potofu yameongezeka kwa kasi, hali inayosababisha madhara mbalimbali katika jamii ikiwa ni pamoja na waumini kuamini miujiza zaidi.

Alisema mataifa ambayo hayajachukua hatua kudhibiti mafundisho hayo ya uongo, ikiwamo Tanzania, yanatakiwa yaweke sheria za kudhibiti usajili wa dini mpya na wachungaji kwa kufuatilia nyendo zao.

"Kwa mchungaji yeyote anayeanzisha dini, sheria hizo zimpime katika mambo mbalimbali, ikiwamo vyeti vya elimu ya theolojia, uchunguzi wa afya ya akili, zifuatiliwe taarifa zao za nyuma kupitia kwa wachungaji pamoja na maaskofu wa makanisa mama wanakotoka.

Kwa kufanya hivyo, tutadhibiti wachungaji kama wale waliosababisha vifo kule Kenya, na wengine," alishauri Padre Dk. Sanga.

Pia alizishauri dini kuungana na kukemea mafundisho ya uongo kwa kuunda chombo cha kukemea mahuburi yasiyo sahihi, kushauri kuwa na chombo cha dini kitakachokuwa na utaratibu wa kupima afya ya akili ya watumishi wa dini kila mara ili kudhiti mambo hasi yanayoweza kujitokeza kutokana na ugonjwa huo kwa wachungaji.

Padre wa Kithodokisia kutoka Mlima wa Kenya, Dk. John Njoroge ambaye pia ni Mjumbe wa Shirika la Makanisa yote Afrika, alisema kutokana na madhara ya upotoshaji kidini yaliyotokea nchini mwake (Kenya), sheria zimeanza kuwekwa kwa lengo la kudhibiti madhara ya aina hiyo.

Alisema shirika hilo lilifanya utafiti mwaka 2019 na kubaini chanzo cha mahubiri potofu kuwa ni wahubiri kutafuta utajiri.

"Lazima serikali zetu ziweke udhibiti kwa wachungaji kutoa mahubiri yanayohimiza sara na kazi na si kuamini katika miujiza na kushinda katika mahubiri na maombi bila kazi.

"Pia serikali zifanye mchakato wa kuwasaidia vijana kupata ajira ili kuondoa wimbi kubwa la vijana wanaokimbilia mahubiri hayo wakifiri ndiyo sehemu sahihi ya kupata ajira," alisema.



Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini Magharibi, Dk. Abednego Keshomshahara. **PICHA: MTANDAO**

# Watakiwa kuendesha biashara kidijitali

**Na Faustine Feliciane**

WAJASIRIAMALI nchini wametakiwa kupanua wigo wa shughuli zao kwa kufanya biashara kidijitali ili kuongeza kipato na kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana wakati wa kutangaza 'Mjasiriamali box' kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo kuendesha biashara zao kimtandao, Mkuu wa kitengo cha biashara wa kampuni ya Tigo, John Sicilima, alisema biashara kwa sasa zinahitaji ubunifu ili kuongeza tija na ndio sababu wengi wanashauriwa kuingia kwenye biashara kwa njia za kidijitali.

"Dunia kwa sasa inahamia kwenye kidijitali, wajasiriamali wadogo na wa kati nao lazima waende na kasi ya teknolojia, kampuni ya simu tunahimiza hivyo kwa vitendo kwa kuleta huduma itakayowasaidia kujiinua na kuchangia kukua kwa uchumi wa nchi," alisema Sicilima.

Aidha, alisema kuwa wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo wametoa ajira nyingi kwa watu na ndio sababu ya kuwashauri kuingia kwenye kufanya biashara kimtandao.

"Kwa sasa karibu asilimia 50 ya ajira nchini zimetoka kwa wajasiriamali, hapa nchini kuna zaidi ya wajasiriamali milioni tatu, kwa picha hii unaweza kuona namna wanavyochangia pato la taifa, kama wataingia kwenye mfumo huu wa kidijitali wataongeza zaidi mapato na kuinua biashara zao," alisema.

# YANGA PRINCESS YAPOTEZA UMAKINI, YAOTA UBINGWA

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya timu yake kukubali kichapo mbele ya watani zao Simba Queens, Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, amesema timu yake ilikosa umakini na kusababisha kupoteza mchezo huo wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania uliochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi.

**Matokeo ya mchezo huo yameifanya Simba Queens kuendelea kukaa kileleni baada ya kufikisha pointi 12, ikishinda michezo yote minne waliyocheza huku nafasi ya pili ikishikiliwa na JKT Queens yenye pointi 10.**

Yanga Princess yenye pointi tatu baada ya kutoka sare mara tatu na kupoteza mechi moja iko katika sanafi ya saba kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 10 kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.

Edna ameliambia gazeti hili licha ya kupoteza mechi hiyo, ameridhishwa na kiwango kilichoonyeshwa na timu yake katika mchezo huo wa watani wa jadi.

Kocha huyo alisema bado wanaendelea kuijenga timu yao na kwa kuangalia kiwango cha mchezaji mmoja mmoja, wameimarika na wanaendelea kuonyesha wako tayari kwa mapambano.

"Kikubwa ni kiwango cha timu, kwangu mimi nafikiri ingekuwa sare, matokeo yangekuwa fair, kutokana na viwango vilivyoonyeshwa na timu zote mbili. Tuko katika kujenga, kuna vitu tunavikosa, lakini tuko katika kujenga timu, kwa bahati mbaya tumekosa umakini, tumejifunga bao, tunahitaji kuendelea kujenga timu,"

Kocha huyo alisema kama anaamini muda bado upo na watarejea tena wakiwa imara katika michezo inayofuata.

"Bado muda upo, tunaweza kupambana na kugombania ubingwa," Edna, nyota wa zamani wa Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), aliongeza.

Naye Kocha Mkuu wa Simba Queens, Yussif Basigi, alisema anajisikia furaha kuwapa wanachama na mashabiki wa timu hiyo furaha.

"Hii ni mara yangu ya kwanza kucheza dabi katika mechi ya ligi, ninafuraha sana kuwapa furaha familia ya Simba, leo (juzi), ni siku kubwa," aliongeza kocha huyo raia wa Ghana.

Esther Mayala, beki wa Simba, alisema walifuata vyema maelekezo ya kocha wao na ndio sababu ya kupata ushindi katika mchezo huo.

Mayala alisema walifahamu Yanga Princess ina wachezaji wenye kasi na ubora mzuri, hivyo walijipanga imara kuwadhibiti na kupelekea kuondoka na pointi tatu muhimu.

Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania itaendelea tena Novemba 19, mwaka huu kwa Simba Queens kuwakaribisha Gets Program kutoka Dodoma, Yanga Princess itawafuata Fountain Gate Princess, JKT Queens itawavaa Ceasiaa, Bunda Queens yenyewe itacheza dhidi ya Mlandizi Queens wakati Alliance Gilrs itakutana na Mashujaa Queens.



Mshambuliaji wa Simba Queens, Elizabeth Wambui (kushoto), akijiandaa kumtoka, nyota wa Yanga Princess, Diana Antwi, katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi. Simba Queens ilishinda bao 1-0. **PICHA: SIMBA SC**

# *Mwembe Makumbi, Kipanga vitani*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAAFANDE wa Kipanga wanatarajia kuwakaribisha Mwembe Makumbi City katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Mao A Visiwani hapa.

Mwembe Makumbi City ndio vinara wa ligi hiyo wakiwa na pointi 22 kibindoni wakati Kipanga yenye pointi 14 wako katika nafasi ya tisa.

Ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), inatarajiwa kuendelea tena kesho kwa KMKM kukutana na KVZ kwenye Uwanja wa Mao A wakati Inter City itawafuata Junguni United kwenye Uwanja wa Finya Arena.

Wakongwe wa Mji Mkongwe, Malindi wao watashuka tena dimbani Novemba 17, mwaka huu kucheza dhidi ya Mwenge FC na New City itawakabili Tekeleza kwenye Uwanja wa Mau B.

Bingwa wa Ligi Kuu Zanzibar hupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati mshindi wa michuano ya Kombe la ZFF hupata nafasi ya kushiriki mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

## Tabora United kuneemeka wakiifunga Simba

**Na Adam Fungamwango**

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Paul Chacha, amesema atatoa kitita cha Sh. milioni 50 endapo kikosi cha Tabora United kitaifunga Simba katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara watakapokutana katika mechi ya mzunguko wa pili.

Chacha alitoa ahadi hiyo katika hafla ya kuwapongeza wachezaji na viongozi wa klabu hiyo baada ya ushindi walioupata wa mabao 3-1 dhidi ya mabingwa watetezi, Yanga uliochezwa Novemba 7, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Kiongozi huyo alisema ushindi huo si wa wachezaji na viongozi tu, bali kwa mkoa wote wa Tabora ambao kwa wiki nzima sasa umekuwa wakipata sifa mara baada ya matokeo hayo.

"Tulikuwa tunatoa kiasi cha Sh. milioni 10 kila wanapopata ushindi, lakini walipoifunga Yanga tuliongeza zawadi kwa sababu wameifunga timu kubwa, tumewapa Sh. milioni 20, tutaitoa mbele za umma ili kila mmoja aone.

Zawadi hii haishii hapo, siku wakimfunga mpinzani mkubwa zaidi, wakimdondosha yule mnyama kubwa yule siku hiyo milioni 50 itawahusu," alisema na kushangiliwa na umati wa wa watu uliojitokeza katika Hospitali ya Rufaa ya mkoa wa Tabora, Kitete, ambako pamoja na mambo mengine ilikuwa ni siku ya kilele cha kumalizia sherehe za ushindi dhidi ya Yanga zilizofanyika mkoani hapo kwa wiki nzima.

Mbali na hafla hiyo, kulikuwa pia na zoezi la kuchangia damu ikiwa ni sehemu ya kusherehekea matokeo hayo ambayo pia yamesababisha Yanga kuhama kutumia Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Tayari, Tabora United imeshacheza dhidi ya Simba katika mchezo wa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa Agosti 18, mwaka huu kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, na kuchapwa mabao 3-0.

Tabora United itaikaribisha Simba katika mchezo wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaofanyika Desemba 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani, Tabora.

Tangu kikosi hicho kiwasili kutoka Dar es Salaam, kikosi hicho kimekuwa kikizungushwa huku na kule mitaani na sehemu mbalimbali mkoani humo kwa ajili ya kupokea pongezi na zawadi kutoka kwa wadau na mashabiki wa soka Tabora ambao walionyesha kufurahishwa na ushindi huo wa kihistoria wa timu yao.

## ZISIKUPITE

### DANILLO ANUKIA UNITED

KOCHA wa Manchester United, Ruben Amorim, anamlenga mlinzi wa Juventus, Danilo, 33, ili awe usajili wake wa kwanza wa Old Trafford katika dirisha la Januari, kwa sababu Mbrazili huyo anamalizia kandarasi yake mwishoni mwa msimu huu. ***(Mirror)***

### DIOMANDE KUTUA ARSENAL

ARSENAL wanamfuatilia mlinzi wa Sporting, Ousmane Diomande, 20, ingawa Chelsea na Bayern Munich pia wanamtaka mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast. ***(Metro)***

### BARCELONA YAMTOSA TRENT

BARCELONA wameondoa nia yao ya kumnunua mlinzi wa Liverpool na Timu ya Taifa ya England, Trent Alexander-Arnold, 26, ili kukidhi matakwa ya mshambuliaji wao chipukizi wa Hispania, Lamine Yamal (17). ***(Football365)***

### ROBERTSON KUULA LIVER

LIVERPOOL inapania kufanya mazungumzo ya mkataba mpya na beki wao wa kimataifa wa Scotland, Andy Robertson, 30, msimu huu wa joto. ***(Football Insider)***

### CITY KIKAANGONI EPL

KLABU za Ligi Kuu England, zimehifadhi haki ya kutafuta fidia kwa mapato yaliyopotea ikiwa Manchester City watapatikana na hatia ya kukiuka kanuni za fedha za ligi hiyo. ***(Times)***

### EDU ALIIKATAA ARSENAL

MKURUGENZI wa zamani wa michezo wa Arsenal, Edu, alikataa mkataba mpya wa kubakia kwa washikabunduki hao ili kuchukua nafasi ya kule kwa mmiliki wa klabu nyingi wa Nottingham Forest, Evangelos Marinakis. ***(Mail)***

### BRANTHWAITE ATAKIWA MAN

KLABU ya Manchester United inapanga kumnunua beki wa Everton na England, Jarrad Branthwaite, 22, msimu huu wa joto. ***(Sportsport)***

### WATATU KUMFUATA AMORIM

KOCHA mpya wa Manchester United, Ruben Amorim, anataka kuwasajili wachezaji watatu wa Sporting, beki wa Ureno, Goncalo Inacio, 23, mlinzi wa Ivory Coast, Ousmane Diomande (20), na mshambuliaji wa Sweden, Viktor Gyokeres (26), ili kuungana nao Old Trafford. ***(Sacha Tavolieri)***

### MAGUIRE: SIONDOKI UNITED

MLINZI wa Timu ya Taifa ya England, Harry Maguire, 31, hana nia ya kuondoka Manchester United ifikapo Januari na anaamini anaweza kupata mkataba mpya kutoka kwa mabosi wa klabu hiyo. ***(TBR Football)***

### PSG YAMFUATA DURAN

KLABU ya Paris St-Germain inajiandaa kuwasilisha ombi la kumnunua mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Colombia, Jhon Duran, 20, ambaye kwa sasa anaitumikia Aston Villa. ***(Fichajes)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# DESCHAMPS AOMBA MBAPPE ASIJADILIWE

**PARIS,** Ufaransa

**Ni baada ya kutojumuishwa katika kikosi cha Ufaransa kuelekea...**

KOCHA wa Ufaransa, Didier Deschamps amesema, Kylian Mbappé, hapaswi kujadiliwa kwa sababu anatakiwa aachwe atulie.

Katika kuelekea mechi hatari ya Ligi ya mataifa ya UEFA dhidi ya Israel itakayochezwa jijini, Paris, Deschamps aliulizwa ikiwa alikuwa amezungumza na Mbappé kuhusu uamuzi wake wa kumwacha katika kikosi chake, fowadi huyo wa Real Madrid.

**Deschamps alitania kwanza alitarajia swali lingeulizwa mapema wakati wa mkutano huo na waandishi wa habari.**

Lakini baadae akajibu: "Sikiliza, nimekwambia nilichokwambia. Uko huru kuzungumza, na kutafsiri hilo. Nina mchezo. Kuna wachezaji 23 hapa. Kylian hayupo, tafadhali mwache atulie."

Mbappé pia hakuwapo katika mchezo uliopita wa Ufaransa kwa sababu ya jeraha dogo la paja.

Kiwango cha Mbappé kimekuwa chini kwa wiki za hivi karibuni baada ya kujiunga na Madrid kutoka PSG msimu wa joto.

Jitihada zake za kuzoea mtindo wa uchezaji wa timu yake mpya zimeambatana na hali mbaya ya klabu hiyo ya Hispania.

Mbappé hajaongeza mabao yake 48 kwa Ufaransa tangu Juni.

Deschamps wiki iliyopita hakufafanua kuhusu chaguo lake la kumwacha Mbappé, lakini alisema haihusiani na ripoti za hivi karibuni katika vyombo vya habari vya Sweden, kuwa nyota huyo wa zamani wa Paris Saint-Germain alikuwa chini ya uchunguzi wa ubakaji.



# AMORIM AFUNGUKA HATASAJILI SPORTING

**MANCHESTER,** England

KOCHA Mkuu mpya wa Manchester United, Ruben Amorim, amesisitiza hatasajili mchezaji yoyote kutoka klabu yake zamani ya Sporting CP kwenye dirisha la usajili la Januari.

Lakini akasema ikimlazimu kusajili mchezaji kutoka kwa waajiri wake hao wa zamani basi atafanya hivyo katika dirisha kubwa la usajili.

Kocha huyo ambaye aliwasii Manchester United Novemba 11, mwaka huu tayari kuanza majukumu mapya ameeleza wachezaji wengi wanaofanya vizuri katika kikosi cha Sporting.

Na pia wanastahili kuwa hapo na kuyafurahia mafanikio ambayo watavuna mwishoni mwa msimu huku akiwatakia mema katika kuumalizia msimu wakati huu ambao yeye ameondoka klabuni hapo.

Kauli za Amorim zimekuja kufuatia tetesi amepanga kuibomoa Sporting ili kuwa na mwanzo mzuri huko Old Trafford lakini Mreno huyo amekanusha taarifa hizo akisema yupo tayari kufanya kazi na wachezaji atakaowakuta ndani ya United.



# Laporte : Nasubiri kutakiwa Madrid

**RIYADH,** Saudi Arabia

BEKI wa Al Nassr, Aymeric Laporte, amesema anaisikilizia simu ya Real Madrid ikiwa wataamua kuhitaji huduma yake na kuongeza ni ngumu kukataa ofa kutoka kwa mabingwa hao wa Ulaya.

Laporte amesema anasikia tetesi za kutakiwa na Real Madrid na anajisikia fahari, lakini kwa sasa anafikiria zaidi kazi yake huko Saudi Arabia.

Real Madrid wanatarajia kusajili beki wa kati kufuatia kukosekana kwa Eder Militao na David Alaba.

Real Madrid imekuwa na majeruhi wengi na hivyo italazimima kuingia sokoni katika dirisha la Januari.

Na Laporte anatajwa yuko katika rada za vigogo hao wa Hispania.

# Spurs kumpa mkataba Son

**LONDON,** England

NAHODHA wa Tottenham Hotspur, Son Heung- Min anatarajiwa kuongeza mkataba mpya na timu hiyo utakaomweka klabuni hapo hadi mwaka 2026.

Mkataba wa sasa unamalizika ifikapo Juni, mwakani na Spurs wanafikiria kumwongezea mwaka mmoja zaidi.

Son alijiunga na Spurs mwaka 2015 akitokea Bayern Leverkusen ya Ujerumani licha ya kuwa mchezaji muhimu na tegemeo kwenye kikosi hicho bado ana ukame wa mataji, lakini anajivunia kucheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2019.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Korea Kusini ana umri wa miaka 32, kiwango chake kimekuwa gumzo barani Ulaya wengi wakiamini anastahili kucheza katika timu zenye uwezo wa kutwaa mataji.



## Simba kurejea kwa kishindo

INATOKA UK. 24

wanaiangalia zaidi Pamba Jiji kwa sababu ndio wanaanza kukutana nayo na itawapa mwanga wa kikosi chake kinapoelekea.

"Tutajikita zaidi kujipanga kuhusu mechi ya CAF baada ya kumalizana na Pamba Jiji. Tunaamini tutafanya kile tunachokitarajia," kocha huyo aliongeza.

Katika mechi za hatua ya makundi, Simba iko Kundi A pamoja na CS Sfaxien ya Tunisia, CS Constatine (Algeria) na Bravos Do Maquis.

## Gamondi akamata faili la Al Hilal CAF

INATOKA UK. 24

dhidi ya Al Hilal kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Oktoba 8, mwaka 2022 katika mchezo wa raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika, shukrani mabao ya Fiston Mayele na Mohamed Abdelrahman, na mchezo wa pili uliochezwa Sudan, ilifungwa bao 1-0 na kutolewa.

Kwa sasa Al Hilal inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu ya Sudan ikiwa na pointi 17, imecheza mechi saba, kushinda tano, sare mbili wakati Yanga yenye pointi 24, iko katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwa pointi moja nyuma ya vinara, Simba.

Wakati huo huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Almasi Kasongo, amesema endapo itabainika mabomba ya sindano yaliyoonekana katika vyumba vya kubadilishia nguo kwenye Uwanja wa Azam Complex, yalitumika kwa ajili ya kuchoma sindano za kuongeza nguvu, timu husika itachukuliwa hatua.

Kasongo alisema ameona video hizo kupitia mitandao ya kijamii na kama ni suala la utumiaji wa dawa za kuongeza nguvu ni haramu.

"Ni haramu kwa wachezaji, kwa viongozi ni haramu, kanuni zetu zinakataza wachezaji, zinakataza viongozi. Pale ambapo watapatikana na hatia, watafungiwa," alisema Kasongo.

Aliongeza bodi yake imelipokea na pale itakapobainika waliofanya walidhamiria kwa nia ovu, hatua zitachukuliwa.

"Kwa sasa hivi ni mapema mno, kwa sababu unaweza kukuta bomba la sindano, na sindano ina kazi nyingi, tumeona, na kuona kwetu imetupa mwanga kujua ni namna gani nzuri tutaliendelea bila kuleta madhara kwa vilabu ambao ndio tunafanya nao kazi, bila kuleta pia madhara kwa mashabiki wetu," aliongeza Kasongo.

# MATAMPI, METACHA, VINARA KUPANGUA PENALTI LIGI BARA

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA Bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita, Ley Matampi, kutoka Coastal Union na makipa wengine watatu akiwamo, Metacha Mnata wa Singida Black Stars wameokoa penalti moja kila mmoja mpaka kufikia raundi ya 10 ya ligi hiyo iliyosimama kupisha Kalenda ya Kimataifa, imefahamika.

Makipa wengine waliookoa penalti ni Hussein Masalanga wa Tabora United na Ramadhani Chalamanda wa Kagera Sugar.

Kwa mujibu wa takwimu za dawati la michezo la Nipashe, makipa hao wamefanya kazi hiyo na kusababisha penalti sita kushindwa kutinga wavuni huku nyingine mbili zikitoka nje.

**Takwimu zinaonyesha jumla ya penalti 25 zimetolewa na waamuzi mpaka sasa, 19 zikiwekwa ndani ya nyavu na sita zikikoswa.**

Matampi, raia wa Jamhuri ya Kidemkokrasi ya Congo, aliokoa penalti ya Djuma Shaaban, katika mchezo ambao timu yake ilicheza Septemba 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam dhidi ya Namungo, ingawa hakuifanya Coastal Union iepuke kupigo cha mabao 2-0.

Metacha alicheza penalti ya Hassan Dilunga wa JKT Tanzania, wakati timu zao zilipokutana Septemba 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Liti mkoani, Singida na kutoka sare ya bao 1-1.

Chalamanda, aliokoa penalti ya Maabad Maulid wa Coastal Union mechi iliyochezwa Septemba 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha, ambao timu yake ya Kagera Sugar ilipoteza kwa bao 1-0.

Masalanga, aliidaka penalti ya Stephane Aziz Ki, Novemba 7, mwaka huu, wakati Tabora United ilipoibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Yanga, mechi ikipigwa kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Penalti mbili ziliota mbawa zilipigwa na Amza Mubarack wa Namungo Agosti 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa, Lindi, timu yake ikipoteza nyumbani kwa mabao 2-0 dhidi ya Fountain Gate, na Heritier Makambo wa Tabora United ilipocheza dhidi ya Fountain Gate na kubugizwa mabao 3-1, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora mechi iliyofanyika Septemba 20, mwaka huu.



Golikipa wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 15 akifanya mazoezi ili kujiandaa na mashindano ya shule ya Afrika kwa mwaka huu yatakayofanyika hivi karibuni nchini Uganda. **PICHA: TFF**

# *Raizin aanika siri ya kung'ara Championship*

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Mtibwa Sugar, Raizin Hafidh, ambaye ameendelea kung'ara katika Ligi ya Championship, amesema siri ya kufanya hivyo ni kufanya mazoezi kwa bidii, kujitunza na kutaka ndoto ya kurejea katika Ligi Kuu itimie, huku akiwa na timu hiyo.

Raizin ambaye ana mabao saba amesema anataka kuonyesha utofauti wa wachezaji waliowahi kutamba na timu kubwa na ambao hawajawahi.

Nyota huyo ambaye aliwahi kutamba akiwa na Coastal Union, Dodoma Jiji na Gwambina, alisema ushindani wa namba kwenye kikosi cha Mtibwa Sugar pia unasababisha kuendelea kupambana ili kupata nafasi ya kuonyesha ubora kwake kwa sababu ana safari ndefu katika maisha ya soka.

"Nimecheza sana Ligi Kuu Tanzania Bara, sasa hivi nipo Ligi ya Championship, ni lazima kwanza kama mchezaji uonyeshe utofauti kwa wewe uliwahi kucheza Ligi Kuu na una levo hiyo, ila tu umekuja huku kwa ajili ya maslahi na si kushuka kwa kiwango.

Pili mimi nafanya mazoezi sana, najitunza, na lengo langu ni kuipandisha daraja Mtibwa Sugar na mimi nirejee tena Ligi Kuu nikiwa na timu hii," alisema Raizin.

Kwa sasa Mtibwa Sugar inaongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 19, ikifuatiwa na Geita Gold yenye pointi 17, zote zikishuka daraja msimu uliopita.

# Michezo

Ijumaa Novemba 15, 2024

Nipashe




Deschamps: Mbappe asijadiliwe UKURASA 21




Kipa wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Aishi Manula, akifanya mazoezi juzi jioni kabla kikosi hicho hakijaondoka nchini jana usiku ili kuelekea Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo), kwa ajili ya mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025), dhidi ya wenyeji Ethiopia itakayochezwa kesho. **PICHA: TFF**

# GAMONDI AKAMATA FAILI LA AL HILAL CAF

## ●●● Ni baada ya kutuma mashushu kuwasoma, mabomba ya sindano...

**Na Adam Fungamwango**

TUMEWAKAMATA, hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, kuelekea mechi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal kutoka Sudan itakayochezwa Novemba 27, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Kabla ya mechi hiyo, Yanga itawakaribisha Fountain Gate katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Novemba 22, mwaka huu.**

Taarifa kutoka Yanga zinasema tayari amenasa mbinu na mifumo yote ya uchezaji wa Al Hilal iliyoko chini ya Mkongomani Florent Ibenge, na ameanza kuifanyia kazi kuelekea mchezo huo wa kwanza wa hatua ya makundi ya michuano hiyo ya CAF.

Chanzo chetu kinaongeza Gamondi alituma wasaidizi wake kwenda kuangalia michezo ya Ligi Kuu Sudan ambayo inafanyika nchini Mauritania na kubaini namna wanavyocheza.

"Kocha (Gamondi), alituma jopo lake kwenda kuangalia baadhi ya michezo ya hivi karibuni ya Al Hilal ambayo inacheza ligi yao nchini Mauritania, tayari wameshamaliza kazi hiyo na kumkabidhi Gamondi taarifa, kwa sasa anatelekeza kwa vitendo kwenye uwanja wa mazoezi," kilisema chanzo chetu.

Taarifa zaidi kutoka Yanga zinasema wanahitaji kupata matokeo mazuri katika mechi zote mbili dhidi ya Al Hilal na kujiweka katika mazingira bora ya kusonga mbele kwenye mashindano hayo ya kimataifa.

Huku akiwakosa baadhi ya wachezaji wake ambao wako katika vikosi vya timu za taiga, Gamondi anaendelea kuongoza mazoezi mara mbili kwa siku, asubuhi wakienda 'gym' na jioni wakifanya mazoezi ya uwanjani ili kujiimarisha kuelekea mechi hiyo.

Hata hivyo, Gamondi amekuwa kimya na akifanya kazi zake kwa vitendo tangu kuwapo kwa tetesi za kutaka kuondolewa katika kikosi cha mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kupata vichapo viwili mfululizo kutoka kwa Azam FC na Tabora United.

Nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, ameliambia gazeti hili wako katika mazoezi 'makali' ya kujiandaa na mchezo huo ambao amesema wanajua utakuwa mgumu kutokana na aina ya wapinzani watakayokutana nayo.

Mwamnyeto alisema anakumbuka waliwahi kutolewa na Wasudan hao mwaka juzi, hivyo safari hii wanahitaji kulipa kisasi.

"Nakumbuka waliwahi kututoa, tukashindwa kuingia katika hatua ya makundi, huu ni wakati wa kulipa kisasi na kuwaonyesha hii siyo Yanga ile," alisema Mwamnyeto.

Beki huyo alisema kocha wao amekuwa akielekeza mikakati ya kukabiliana na timu hiyo ambayo imekuwa ikifanya vyema katika michuano hiyo.

Yanga ilitoka sare ya bao 1-1

INAENDELEA UKURASA 23

# Simba kurejea kwa kishindo

**Na Faustine Feliciane**

KATIKA kuhakikisha wanajiimarisha kileleni, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema wanatarajia kurejea kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara watakapoifuata Pamba Jiji ya FC ya jijini, Mwanza kwa kishindo.

Pamba Jiji FC itaikaribisha Simba katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Novemba 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Kirumba.

Siku nne baada ya mechi hiyo, Simba itacheza mchezo wa kwanza wa hatua ya makundi wa mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho dhidi ya Bravos do Maquiz kutoka Angola itakayochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Fadlu, alisema wamejipanga kurejea katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa imara kwa sababu wanataka kujiweka vizuri na kuimarisha morali ya wachezaji kuelekea mechi hiyo ya kimataifa.

Fadlu alisema mechi hiyo dhidi ya Pamba Jiji itakuwa sehemu ya maandalizi ya kuwakaribisha Waangola na wanawaomba wanachama na mashabiki wa Simba kujitokeza kwa wingi kuwashangilia.

"Ninawaomba mashabiki wa Mwanza na sehemu nyingine wajitokeze kwa wingi, ni mchezo muhimu sana kwetu kuelekea katika mechi yetu ya Kombe la Shirikisho Afrika, ushindi utaongeza morali na hamasa kubwa kwa wachezaji wetu," alisema Fadlu.

Kocha huyo alisema pia kwa sasa wapo katika maandalizi ya mchezo huo wa Ligi Kuu sambamba na kujipanga kuwakabili Bravos do Maquis kwa sababu michezo yote wanaichukulia kwa umuhimu mkubwa.

"Ushindi dhidi ya Pamba Jiji utazidi kutuimarisha kileleni katika msimamo, lakini ushindi kwenye mchezo wa kimataifa utatufanya tuwe na mwanzo mzuri katika kundi letu, hivi vyote vinahitaji umakini na kujituma kwa wachezaji wangu," Fadlu alisema.

Aliongeza licha ya kuufikiria mchezo wa mashindano ya kimataifa, Fadlu alisema kwa sasa

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >